**RC** aagiza mchakamchaka kwa shule zote

UKURASA 2



**WAGOMBEA** wa udiwani 127 kupigiwa kura leo kata 22

UKURASA 4

**WAKALA** Misitu kupanda miti tiba saratani

UKURASA 4


# Nipashe

Jumatano Machi 20, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581621

www.ippmedia.com

MWANG… JAMII

www.twitter.com/nipashetz

Maoni@nipashe.co.tz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




**REAL MADRID YALALAMIKIA UBAGUZI KWA VINICIUS**

UKURASA 22

## MUME AKIENDA JELA MIAKA 60

# Magumu walioachiwa mke, watoto watano



**NI** aliyenajisi na kumpa ujauzito mwanawe wa miaka 11. Uk. 2

Nyumba anayoishi Wivina Felician (picha ndogo), watoto wake watano na mjukuu, Gongo la Mboto, jijini Dar es Salaam.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dhahabu ya Bil. 1.5/- yanaswa ikitoroshwa



UKURASA 5

Waziri wa Madini, Anthony Mavunde (kulia) na Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, SACP Benjamin Kuzaga, wakionyesha sehemu ya vipande zaidi ya 300 vya dhahabu vyenye uzito wa kilogramu 9.8 kwa waandishi wa habari, jijini Mbeya jana, iliyokamatwa ikitoroshwa, ambapo watu 10 wanashikiliwa. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Operesheni ya vidhibiti mwendo kwa malori yaja

UKURASA 3

**MICHEZO** **GAMONDI AICHAMBUA MAMELODI KWA YANGA** UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Wafuasi wa Chama cha ACT-Wazalendo Mkoa wa Lindi, wakiwa kwenye maandamano ya kumpokea Mwenyekiti mpya wa chama wa mkoa huo, Isihaka Mchinjita, mjini humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

MUME AKIENDA JELA MIAKA 60

# Msuguano wamwachia maisha mapya mama, watoto watano

**Na Mwandishi Wetu**

HUU ndio ulimwengu mpya wa maisha ya Wivina Felician (35), mkazi wa Gongo la Mboto, jijini Dar es Salaam:

Ndani ya chumba cha nyumba ya kupanga, mama huyo anaishi na wanawe watano - watatu wa kike (mkubwa ana umri wa miaka 13 na mdogo wao wa mwisho ana umri wa miaka miwili). Pia ana mjukuu ambaye ni zao la ukatili wa kijinsia. Ni mtoto wa mumewe.

Kula kwao kunategemea mauzo ya biashara yake ya vitafunwa na kuna siku wanashindia mlo mmoja; kodi ya chumba ya miezi sita aliyolipiwa na Kituo cha Taarifa na Maarifa (KC) inafika ukomo mwezi ujao.

Mumewe ambaye ndiye chanzo cha madhila hayo, yuko gerezani, anatumikia kifungo cha miaka 60 baada ya kupatikana na hatia ya kunajisi mwanawe wa kambo Novemba, 2023.

Awali, mumewe, Mrisho Hodari (45) alishtakiwa kwa kunajisi wanawe wawili wa kambo, lakini ushahidi haukumtia hatiani kwa mtoto wa kwanza.

Katika mazungumzo na mwandishi wa habari hizi nyumbani kwake Gongo la Mboto jana, mama huyo alirejea yaliyomsibu, hata kuishi maisha magumu.

Alidai kuwa mumewe huyo alimpa ujauzito yeye pamoja na mwanawe wa kwanza (jina halikutajwa) aliyempata kwa mwanamume mwingine kabla hawajaoana na Mrisho.

Mama huyo alidai bintiye huyo alipata ujauzito akiwa na umri wa miaka 11 na kujifungua mtoto wa kiume, wakipishana miezi miwili tu yeye na mwanawe huyo kujifungua.

Mama huyo anayeishi Kata ya Majohe, kwa sasa analea familia ya watu saba; wanawe watano, mjukuu na yeye mwenyewe.

"Ninatakiwa nilishe familia milo yote na kuwapa wanangu mahitaji maalum kama wanavyopata watoto wengine. Mwanangu mdogo, bado ana umri wa miaka miwili, anayefuatia anasoma chekechea, mwingine darasa la tatu na mwingine la nne, wote wanahitaji kula na kupata vifaa vya shule kwa wakati mmoja," alilalama Wivina.

Ndani ya chumba hicho kisichokuwa na huduma ya umeme anamoishi mama huyo na familia yake, mwandishi wa habari hizi aliona mna godoro lenye ukubwa wa futi tano kwa sita ambalo limewekwa chini, hakuna kitanda. Hapo ndipo mama huyo hulala na wanawe wote watano na mjukuu.

Sakafu ya chumba hicho anacholipia Sh. 15,000 kwa mwezi, imebomoka na kuna baadhi ya sehemu kuna mashimo. Kipato chake kinategemea biashara ya kuuza vitafunwa. Hakikidhi mahitaji yake kwa sasa kutokana na familia kuwa kubwa na mahitaji kuwa mengi.

"Kulingana na biashara ninayofanya. ninashindwa kukidhi mahitaji ya familia yangu kwa wakati, watoto watatu wanakwenda shule, wana mahitaji yao nje na kula au kulala, wanahitaji madaftari, sare za shule na mahitaji mengine ambayo muda mwingine ninashindwa kuwatimizia kutokana na hali ngumu ya maisha niliyonayo.

"Ninawaomba Watanzania na wanajamii wenzangu wanisaidie angalau nyumba ya kukaa na mtaji ili nikidhi mahitaji ya familia yangu.

"Nyumba itanisaidia kuondokana ma kero za kuwaza kudaiwa kodi mara kwa mara ili angalau basi hata biashara nitakayokuwa ninaifanya nione faida yake na kuhudumia familia yangu," alisema.

Alibainisha kuwa mwanawe wa kwanza sasa yuko katika mafunzo ya ufundi cherehani, akifadhiliwa na KC huko Majohe, jijini.

Kituo hicho kinajishughulisha na kutoa elimu ya ujasiriamali kwa kinamama na vijana, kikianzisha kikundi kinachozalisha bidhaa mbalimbali kama vile mbolea itokanayo na mboji, chakula cha kuku, batiki, kulima bustani na uzalishaji wa sababu kwa ajili ya kufulia.

KC pia inashirikiana na Mtandao wa Jinsia nchini (TGNP) kusaidia jamii, hasa wanawake na watoto wenye changamoto za unyanyasaji wa kijinsia katika kata hiyo, hata kutoa msaada wa kisheria kama ulivyofanya kwa mama huyo wakati kesi dhidi ya mumewe ilipokuwa inaendelea mahakamani.

Mwenyekiti wa KC, Tabu Ally, alisema kituo chao kilitoa msaada kwa mama huyo wakati wa kesi kuhakikisha anapata haki yake mahakamani.

"Kituo chetu kilikuwa kinampatia nauli ili aweze kwenda mahakamani Lugoba, mkoani Pwani. Pia tulimpatia mtu ambaye alikuwa akimsindikiza mahakamani hadi kesi ilipoisha.

"Vilevile, tulimpatia godoro hilo la tano kwa sita ambalo analitumia kwa sasa kulala na watoto wake ili angalau waweze kujihifadhi," alisema.

Tabu alisema alitoa wito kwa jamii kumsaidia mama huyo kwa kuwa changamoto anazopitia ni kubwa na hana msaada kwa sasa, zaidi ya kutegemea biashara yake ya kuuza vitafunwa.

"Sisi kama kituo hatuwezi kumsaidia kila kitu, kwani wenye changamoto kama hizo nao ni wengi katika jamii, tunawagawia kidogo tunachopata," alisema.

Mwenyekiti wa KC huyo pia alieleza changamoto wanazokutana nazo katika utekelezaji majukumu yao, ikiwa ni pamoja na ushirikiano hafifu kutoka kwa jamii inayokumbana na changamoto za unyanyasaji wa kijinsia.

Pia alisema wanahitaji kupata nyumba itakayotumika kuwapa hifadhi waathirika wa matukio ya ukatili wa kijinsia. Kwa sasa, utaratibu waliowekwa kwa kiwango chao, wakipata mtu mwenye changamoto za aina hiyo, huwa anapewa hifadhi ya nyumbani kwa mwenyekiti huyo.

Alibainisha kuwa kituo hicho kwa kushirikiana na TGNP, hadi kufikia mwaka jana (2023), wameshasaidia kutatua kesi 60 (15 za ulawiti, 25 za ndoa, 15 za vipigo kwa wanawake na tano za ubakaji watoto).

"Tangu kituo hiki kianzishwe mwaka 2018, tumeshasaidia jamii kutatua changamoto katika kesi zaidi ya kesi 100 katika kata hii ya Majohe," Tabu alihitimisha.

# RC aagiza utaratibu wanafunzi kukimbia mchakamchaka kabla kuingia darasani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, ameagiza shule zote mkoani hapa, kuweka utaratibu wa wanafunzi kukimbia mchakamchaka ili kuwasaidia kuwa na afya, ukakamavu, uzalendo na kujiepusha na magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Senyamule, alisema hayo jana jijini hapa, alipokuwa akizindua Wiki ya Wadau wa Elimu jijini hapo.

Alisema, hakuna mwanafunzi anayeweza kufanya vizuri kwenye masomo yake kama hayuko sawa kiafya, na mazoezi ndiyo njia pekee ya kuimarisha afya.

"Kupitia jukwaa hili la wadau wa elimu Mkoa wa Dodoma niagize shule zote mkoani hapa kuhakikisha zinaweka utaratibu mzuri wa wanafunzi kukimbia mchakamchaka kabla ya kuanza masomo kwa umbali fulani ili kuwafanya wanafunzi kuwa wenye afya," alisema Senyamule.

Aidha, alisema mchakamchaka unafaida nyingi ikiwamo kuwafanya wanafunzi kuwa wenye akili na wazalendo kupitia nyimbo watakazoimba wakati wakikimbia kuwakumbusha historia ya nchi yao.

"Pamoja na faida hizo, lakini mnapokimbia mnaimba nyimbo ambazo zinawajenga wanafunzi kuwa wazalendo na kuwakumbusha historia ya taifa lenu lini hata hapo baadaye tuwe na wananchi wanalolifahamu vizuri taifa lao," alisema.

Alisema hivi sasa kumekuwapo na idadi kubwa ya watu wanaosumbuliwa na magonjwa yasiyo ya kuambukiza ambayo kwa kiasi kikubwa yanasababishwa na kutofanya mazoezi.

"Mazoezi ni muhimu sana kwetu kwani hivi sasa wapo watu wengi wanasumbuliwa na magonjwa yasiyo ya kuambukiza, lakini kama tutafanya mazoezi tunaiondolea mzigo serikali kwa kuhudumia wagonjwa.

"Naagiza shule zote mkoani Dodoma zinaweka maeneo ya kufanya mazoezi ili kutoa fursa kwa wanafunzi kufanya mazoezi yatakayosaidia kuimarisha afya zao na kuwalinda na magonjwa mbalimbali," alisema.

Baadhi ya wakazi wa Mkoa wa Dodoma wameunga mkono agizo hilo, wakisema kuwa ni jambo sahihi kwa kuwa mchakamchaka ni sehemu sahihi ya kujengea ukakamavu wanafunzi.

Chritopher Dioni, mkazi wa jijini hapa, alisema anaungana na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma kwa kuwa hata wao wakati wakiwa wanafunzi walikuwa wanakimbia mchakamchaka ambao uliwasaidia kufanya mazoezi kabla ya kuanza masomo ya kila siku.

"Mchakamchaka unamsaidia mwanafunzi kujiweka sawa kiakili kabla ya kuingia darasani, lakini pia unaimarisha afya yake tofauti na hivi sasa ambapo shule nyingi watoto wanaletwa na gari halafu hawana muda kabisa wa kufanya mazoezi," alisema.

Naye Sekela Kilembe alisema, wanafunzi wa miaka ya nyuma mchakamchaka uliwajenga kuwa wakakamavu na kuwafanya wazalendo kutokana na nyimbo walizokuwa wanaimba kuwakumbusha historia za nchi yao na bara la Afrika.

Awali, Ofisa Elimu wa Mkoa wa Dodoma, Vicent Kayombo, alisema Wiki ya wadau wa elimu iliyozinduliwa jana itatumika kujadili changamoto na kuleta mageuzi makubwa kwenye sekta ya elimu mkoani hapa.

# Malori kufungwa vidhibiti mwendo kudhibiti ajali

Na Christina Mwakangale

KAMANDA wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, DCP Ramadhani Ng'anzi, ametangaza operesheni mpya ya mwendokasi na mwenendo wa malori, sasa yatakuwa na mfumo wa ufuatiliaji mwendo na mwenendo (VTS).

Aidha, amesema operesheni ya kuondoa namba aina ya 3D kwenye magari, zilizopigwa marufuku imekamata magari 704 nchini, huku Mkoa wa Dar es Salaam, ukiwa kinara.

Kamanda Ng'anzi, aliyasema hayo kwenye mazungumzo maalum na Nipashe, kuhusu masuala mbalimbali ya usalama barabarani, ikiwamo elimu kwa watumiaji wa vyombo vya moto wakiwamo madereva na watembea kwa miguu.

Kuhusu magari yaliyokamatwa yakiwa na namba hizo, mkoani Dar es Salaam ni 256 kati ya 704 nchi nzima, huku Wilaya ya Temeke ikiongoza kwa kukamata magari 134 na Ilala yakishikiliwa 122.

"Kuna mikoa ambayo hakukuwa na magari yaliyokamatwa yakiwa na 3D ambayo ni Katavi, Simiyu na Mara. Mikoa mingine yote iliyobaki ilikuwa na magari yenye namba hizo kwa idadi tofauti," alifafanua.

Kadhalika, alisema hivi karibuni magari makubwa yakiwamo malori ya mizigo yatawekewa mfumo wa ufuatiliaji mwendo na mwenendo (Vehicle Tracking System-VTS), ambao utawafuatilia madereva wa magari hayo wakiwa barabarani.

"Mfumo wa VTS umesaidia kufuatilia 'speed' yaani mwendokasi na mwenendo 'behaviour' kwa mabasi. Mfumo huu umefungwa makao makuu hapa (Dar es Salaam) na kila makao makuu ya mkoa. Kila basi la abiria linafuatiliwa control room yetu.

"Madereva wa mafuso wanaoleta bidhaa kama nyanya Kariakoo, wanasafiri usiku wanakimbia sana. Baadaye tunafikiria kuwafungia mfumo huo wenye malori," alisema Kamanda Ng'anzi.

Pia alisema kikosi hicho kimeendelea kutoa elimu nchini, kuendeleza stadi, uwezo na maarifa barabarani ili kupambana na ajali, kwa kuwafuata madereva kwenye vijiwe vyao wakiwamo wa bodaboda.

"Tumelenga makundi mengi, watembea kwa miguu, kuwapa kanuni za kuvuka barabara, tahadhari za kuchukua wawapo barabarani na namna ya kuwashika watoto wakiwa wanatembea, avuke maeneo gani na asivuke maeneo gani. "Madereva ni kundi ambalo tunakaa nalo wachukue tahadhari na tunawaambia wanapokuwa barabarani waendeshe gari zaidi ya moja analoliendesha, lazima ujue gari lako na ujue dereva wa mbele, nyuma, pembeni yako ana tabia gani," alisema Kamanda Ng'anzi.

Pia alisema kuna maelekezo hupewa madereva kama kuchukua tahadhari na wanapowaona watoto pembezoni mwa barabara, kwa kuwa uamuzi wao huwa ya papo hapo, huweza kuvuka kwenda upande wa pili wa barabara ghafla.

"Unapokuta kundi la watoto lazima upunguze mwendo, unapokaribia makazi ya watu lazima upunguze mwendo, tunawafundisha kuepuka mwendokasi kwa sababu ni chanzo cha ajali na inapotokea ajali madhara yake huwa ni makubwa, tofauti na lililo kwenye mwendokasi, mdogo," alisema Kamanda Ng'anzi.

Akifafanua kwa madereva, ni kuwa na uvumilivu, subira na kutochukua uamuzi wa sekunde chache ambao utauathiri jamii kwa ujumla na si dereva mmoja.

"Mfano ukatambua dereva anayekuja mbele yangu ameshakosea, nimpishe kwanza apite, halafu utakuwa umeepusha madhara mengine, kila dereva akiwa na udereva wa kujihami, ajali nyingi zitaepukika," aliongeza.

Alisema kundi lingine linaloongoza kutajwa kuwa ni kero na lenye usumbufu katika matumizi ya barabara ni madereva wa bodaboda, ambao hivi sasa wamewekewa mabalozi pamoja na walezi kutoka jeshi hilo.

"Baada ya operesheni ya 3D na ving'ora, muda si mrefu tunawageukia bodaboda ambao wanatajwa kuwa ni kero barabarani. Dawa yao inachemka. Tutapambana nao kwa kuwataka wavae kofia ngumu 'helmet', waache kupakia mishikaki (kubeba abiria zaidi ya mmoja) na wawe la leseni muda wote.





Kadhalika, miongoni mwa watumiaji wa barabara hasa madereva wa vyombo vya moto, wanaoongoza kwa makosa ya usalama wa barabarani ni madereva bodaboda, ambao kwao kuvuka taa nyekundu, ni jambo la kawaida.

"Ninawataka bodaboda wabadilike tabia yao, fikra na mtazamo wanapotumia barabara, opersheni yao inakuja, tutaizuia pikipiki yake na tutamkamata anayepakia mshikaki na aliyepakiwa mshikaki, kwanini ukubali, ni kama abiria aliyepanda katika gari na kuning'inia," alisema.

Kamanda alisisitiza kundi lingine linalolengwa katika elimu ni watembea kwa miguu, ambao wanapewa elimu ya namna ya kutumia barabara na kuchukua tahadhari.


Kamal

KAMAL GASES LIMITED

TAARIFA KWA UMMA

Sisi **Kamal Gases limited** wazalishaji namba moja wa gesi za viwandani zenye ubora uliothibitika na Shirika la viwango Tanzania TBS.

Tumegundua kuwepo kwa wazalishaji wa gesi wanaotumia mitungi yenye nembo ya KGL kinyume na sheria.

Tunawatangazia wazalishaji, watumiaji wa gesi za viwandani na umma kwa ujumla kwamba ni kinyume cha sheria kujaza, kuuza, na kusambaza gesi iliyowekwa kwenye mitungu yenye nembo ya kamal ambayo haikuzalishwa na Kamal Gases Limited.

Hivyo mnahabarishwa kwamba; Kamal Gases Limited wapo katika zoezi kabambe la kufuatilia na kukamata wahusika wote wanaozalisha gesi za viwandani na kujaza katika mitungi yenye nembo au alama ya kamal gases limited kinyume cha utaratibu.

Kamal Gases Limited itachukua hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufungua kesi za madai na jinai kwa yoyote atakaye tumia mitungi ya gesi yenye nembo ya Kamal Gases Limited kujaza gesi aliyoichakata mwenyewe au iliyochakatwa na wazalishaji wengine nje ya Kamal Gases Limited

Tunatoa wito kwa wateja wetu kuendelea kutumia huduma ya gesi ya Kamal Gases Limited kwa kupitia vituo vilivyoidhinishwa na kuitambulika na Kamal Gases Limited au wafike kiwandani chang'ombe industrial area plot no. 188/2 kwa maelezo zaidi piga simu namba **+255 765 169 444**

**Imetolewa na**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Kamal Gases Limited**
**Dar es Salaam**

21780802

# Wakala Misitu kupanda miti ya tiba ya saratani

Na Elizabeth Zaya

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) umeanza mkakati wa kupanda miti dawa ambayo mbali na magonjwa mengine, itatumika kutibu magonjwa ya saratani, ikiwamo tezi dume.

Kamishna wa Uhifadhi wa TFS, Prof. Dos Santos Silayo, alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa mkutano ulioshirikisha wahariri na waandishi wa habari.

Prof. Silayo alisema tayari upandaji miti hiyo umeshaanza hususani katika milima ya mashariki mwa nchi na sehemu zenye miinuko mikubwa kama Kilimanjaro, Mbeya na Rukwa.

Alisema mkakati huo ni sehemu ya utekelezaji maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuwa na mpango wa kupanda miti nchi nzima kwa ajili ya kutunza mazingira hususani miti dawa.

"Hifadhi zetu za misitu zina mtawanyiko mkubwa sana wa baionuai za mimea na wanyama. Kwenye mimea tunafahamu dawa nyingi za kutibu binadamu chanzo chake kikubwa kinatokana na mimea, hapa Tanzania tuna bahati kwamba tunayo mimea mingi sana hususani katika Mlima wa Tao la Mashariki, (una miti) ambayo inatumika kutoa dawa za kutibu magonjwa mbalimbali.

"Kwa hiyo, ili kuongeza mchango wa sekta ya misitu katika huduma kwenye sekta hii ya afya, sisi kama TFS tunaongeza kilimo cha miti hii katika mpango mkakati wetu wa upandaji miti," alisema.

**MAFANIKIO**

Pamoja na mambo mengine, Prof. Silayo alitaja mafanikio 12 ambayo TFS imeyapata katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan. Alisema TFS inasimamia rasilimali watu wanaojumuisha maofisa 643 na askari 1,454, jumla yao ni 2097. Katika kipindi cha mwaka 2020/21-2023/24, TFS iliajiri watumishi wapya 495, huku watumishi 180 wakipatiwa mafunzo ya muda mrefu na watumishi 1,481 ya muda mfupi katika fani mbalimbali.

Alitaja mafanikio mengine kuwekwa mikakati ya kujikinga na moto pori katika hifadhi za misitu ambayo walifanya kwa kusafisha mipaka na njia za moto zenye urefu wa kilomita 13,426.

Prof. Silayo alisema walitoa mafunzo ya mbinu za kukabiliana na kuepusha matukio ya moto kwa wananchi zaidi ya 29,685 katika vijiji 749 vinavyozunguka misitu 120 na walianzisha na kutoa mafunzo kwa vikosi vya kukabiliana na matukio ya moto vyenye watu 365. Alisema katika kukabiliana na majanga ya moto, walikarabati minara 21 ya kuangalizia moto katika mashamba ya miti na kuimarisha matumizi ya mitambo ya kuzimia moto na mfumo wa satelaiti wa kubaini matukio ya moto mapema.

"Kutokana na juhudi hizo, matukio ya moto yalipungua kwa asilimia 11," alisema Prof. Silayo na kulitaja ongezeko la viwanda vya kati hadi vikubwa kutoka 6,029 hadi 7,356 sawa na ongezeko la asilimia 18, ni mafanikio mengine kwa wakala huo.

Alifafanua kuwa viwanda hivyo vinajumuisha vidogo vya kutengeneza samani, uchakataji mbao, utengenezaji bidhaa za ujenzi kama vile marine boards, veneer; viwanda vya nishati ya mkaa, viwanda vya nguzo hadi vile vikubwa vya kutegeneza karatasi.

Prof. Silayo pia alisema ufugaji na uzalishaji asali ni sehemu ya mafanikio walilolipata katika kipindi cha miaka mitatu; uzalishaji mazao ya nyuki nchini umeongezeka hadi kufikia wastani wa tani 32,691 kutoka tani 31,179 sawa na ongezeko la asilimia tano.

Alisema kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita, Tanzania imeuza tani 5,000 za asali nje ya nchi yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 40.

"Asali ya Tanzania hupimwa katika maabara za kimataifa za ithibati kila mwaka. Kwa miaka yote tumepata alama za juu wastani 96/100. Masoko makubwa yako nchi za Jumuiya ya Umoja wa Ulaya, Uarabuni, Marekani na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Nchi Kusini mwa Afrika (SADC),

"Pia kupitia mashindano ya ubora wa asali zinazozalishwa Afrika, asali ya Tanzania iliyozalishwa mkoani Tabora ilishika nafasi ya pili kwa ubora," alitamba Prof. Silayo.

Kwa mujibu wa kamishna wa uhifadhi huyo, katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Samia, TFS imekusanya Sh. bilioni 371.9, ikiwasilisha katika Mfuko Mkuu wa Serikali Sh. bilioni 62.9 za asilimia 15 ya makusanyo yake.

Kamishna Silayo alisema idadi ya watalii waliotembelea vituo vya utalii ikolojia pia iliongezeka kutoka 59,606 mwaka 2020/21 hadi 242,824 mwaka 2022/23.






## Wagombea wa udiwani 127 kupigiwa kura leo kata 22

Na Mwandishi Wetu

WAGOMBEA udiwani 127 kutoka vyama 18 vya siasa wanatarajiwa kupigiwa kura katika uchaguzi mdogo kata 22 za Tanzania Bara unaofanyika leo.

Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Jaji (Rufani) Jacobs Mwambegele alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akitoa risala ya uchaguzi huo.

Jaji Mwambegele alisema kati ya wagombea hao 127, wanaume ni 89 na wanawake ni 38; wapigakura 128,157 walioandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapigakura watashiriki katika uchaguzi huo na jumla ya vituo 373 vya kupigia kura vitatumika.

"Tume inatoa pongezi kwa wadau wote wakiwamo wapigakura na wananchi katika kata 22 zenye uchaguzi kwa utulivu walioonesha wakati wote wa kipindi cha kampeni," alisema Jaji Mwambegele.

Alisema wasimamizi wa uchaguzi katika kata husika wamekamilisha taratibu zinazoweka mazingira yanayowawezesha mawakala wa vyama vya siasa kufuatilia mchakato mzima wa uchaguzi. "Mawakala wanawajibika kulinda maslahi ya vyama na wagombea wao na katika utekelezaji majukumu yao vituoni, wanapaswa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu za uchaguzi na maelekezo ya tume," alifafanua Jaji Mwambegele.

Aliwataka wapigakura katika uchaguzi huu mdogo kujitokeza kwa wingi kwenye vituo vya kupigia kura leo, ili kuchagua viongozi wanaowataka huku akikumbusha vyama vya siasa, wagombea na wadau wengine wa uchaguzi kujiepusha na vitendo vinavyoashiria uvunjifu wa amani.

"Mafanikio ya uchaguzi huu yatatokana na kuwapo hali ya utulivu na amani katika maeneo yote yenye uchaguzi. Hivyo, tume inatarajia kuona hali ya amani na utulivu iliyopo sasa inaendelea kuwapo hadi shughuli za uchaguzi zitakapokamilika," alisema Jaji Mwambegele.

Alitaja mambo mengine ambayo hayaruhusiwi kufanyika baada ya jana saa 12:00 na siku ya uchaguzi kuwa ni pamoja na kutumia alama za vyama vya siasa zinazoashiria kampeni kama vile vipeperushi, bendera na mavazi na upigaji kura katika maeneo yote ya uchaguzi, utafanyika katika vituo vilevile vilivyotumika wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.

Alisema vituo vya kupigia kura vitafunguliwa saa 1:00 asubuhi na kufungwa saa 10:00 jioni. Iwapo, wakati wa kufunga kituo watakuwapo wapigakura katika mstari ambao wamefika kabla ya saa 10:00 jioni na hawajapiga kura, wataruhusiwa kupiga kura na mtu yeyote hataruhusiwa kujiunga katika mstari wa wapigakura baada ya saa 10:00 jioni.

"Watakaoruhusiwa kupiga kura ni wale tu ambao wamo kwenye Daftari la Kudumu la Wapigakura kwenye kata husika na wana kadi zao za mpigakura.

"Hata hivyo, tume kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 62 (a) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, imeruhusu wapigakura ambao wamepoteza kadi zao au kadi kuharibika kutumia vitambulisho mbadala kama vile pasi ya kusafiria, leseni ya udereva au kitambulisho cha uraia kinachotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), mradi majina yaliyopo katika vitambulisho hivyo, yawe sawa na yaliyokuwapo katika kadi ya mpigakura," alifafanua Jaji Mwambegele.

Kata zinazofanya uchaguzi ni Kimbiji (Kigamboni), Kasingirima (Kigoma/Ujiji), Ndevelwa (Tabora), Mshikamano (Musoma), Msangani (Kibaha), Utiri (Mbinga), Fukayosi (Bagamoyo), Mlanzi (Kibiti) na Mbingamhalule (Songea).

Kata nyingine ni Isebya (Mbogwe), Kibata (Kilwa), Busegwe (Butiama), Kamwene (Mlimba), Chipuputa (Nanyumbu), Buzilasoga (Sengerema), Mhande (Kwimba), Kabwe (Nkasi), Bukundi (Meatu), Mkuzi (Muheza) na Boma, Mtimbwani na Mayomboni (Mkinga).



Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zubeir Ali Maulid (kushoto), akizungumza wakati wa hafla ya futari iliyoandaliwa na Benki ya NBC, kwa ajili ya wateja wake, mjini Zanzibar mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dhahabu ya bil. 1.5/- yanaswa ikitoroshwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHEHENA ya dhahabu yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 1.5 imenaswa mkoani Mbeya ikitoroshwa kwenda kuuzwa kusikojulikana, watu 10 wanashikiliwa na vyombo vya ulinzi na usalama wakituhumiwa kuhusika na utoroshaji huo.

Dhahabu hiyo yenye uzito wa kilogramu 9.8 inadaiwa kukamatwa na Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Kikosi Kazi cha Kuzuia utoroshaji madini ikiwa inaandaliwa kusafirishwa na watu hao.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mjini hapa, Waziri wa Madini, Anthony Mavunde alisema watu hao walinaswa kwenye moja ya nyumba zilizoko katika Mtaa wa Ilomba, jijini Mbeya kufuatia operesheni maalumu iliyofanywa na vyombo hivyo.

Alisema shehena hiyo ilikuwa imegawanywa kwenye vipande 334 ambavyo vilikuwa vimehifadhiwa kwenye vyombo maalum na kwamba watu hao walikutwa na vifaa mbalimbali vilivyokuwa vinatumika kuandalia dhahabu hiyo.

Alivitaja baadhi ya vifaa hivyo kuwa ni mizani za kisasa za kupima uzito na ubora wa dhahabu, vifaa vya kuchomea dhahabu, mitungi ya gesi, vifaa vya kupoozea dhahabu na kemikali maalum ya kusafishia dhahabu.

"Watu hawa endapo wangefanikiwa kutorosha dhahabu hii, serikali ingepoteza zaidi ya Sh. milioni 144 ambazo ni mrabaha, ada ya ukaguzi, Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na Ushuru wa Huduma wa Halmashauri," alisema Mavunde.

Aliwataka wamiliki wa nyumba za kupangisha kuhakikisha wanawafahamu wapangaji wao pamoja na shughuli wanazofanya ili kuepuka kupangisha watu wabaya na hivyo kuwasababishia matatizo. Sheria ya Uhujumu Uchumi inaelekeza kutaifisha mali, ikiwamo nyumba za wanaokutwa na hatia.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga alisema maofisa wa vyombo vya ulinzi na usalama walipofika kwenye nyumba hiyo kuliibuka purukshani zisizo za kawaida.

Alisema kuwa baada ya wahalifu hao kuzidiwa nguvu na maofisa hao, baadhi walikimbilia kwenye dari na vipande hivyo vya dhahabu, lakini wakanaswa kutokana na maofisa hao kutumia mbinu na medani za kijeshi.

Alisema baada ya watu hao wote kukamatwa, nyumba hiyo ilipekuliwa na kukutwa vipande hivyo vya dhahabu na vifaa mbalimbali ambavyo watuhumiwa hao walikuwa wanavitumia kuandalia dhahabu hizo.

"Hawa maofisa wetu wote wana mafunzo maalum ya kukabiliana na uhalifu na ndio maana hawa wahalifu pamoja na kupanda darini, bado walikamatwa na kutiwa nguvuni, ilitumika mbinu ambayo siwezi kuitaja hapa maana hawa watu walikuwa wabishi," alisema Kamanda Kuzaga.

Mwenyekiti wa Mtaa walipokamatwa watuhumiwa hao, Subira Sanga, alisema watu hao walikuwa hawafahamiki kwenye mtaa wake kutokana na kupangishwa nyumba bila kutambulishwa kwa viongozi.

Alisema yeye binafsi aliwafahamu siku moja kabla ya kukamatwa baada ya kuwaona wakitoka ndani ya nyumba hiyo na alipohoji kuhusu utaratibu uliowaingiza katika nyumba hiyo pamoja na shughuli wanazofanya, wakajitambulisha kuwa wanafanya biashara ya mazao.

Alisema aliwaelekeza kufuata utaratibu wa kwenda kujitambulisha ili waendelee kuishi katika eneo hilo na wakaahidi kutekeleza, lakini wakakamatwa ndipo akabaini walikuwa wahalifu.

Mmiliki wa nyumba hiyo iliyoko eneo la Ilomba, Vitus Sanga alisema wakati wanaomba kupangishwa nyumba hiyo, walijitambulisha kwake kuwa walikuwa wanafanya biashara ya mazao na walikuwa wawili tu, hakujua kuwa walikuwa wanaishi 10 na wanafanya shughuli ambayo ni haramu. Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Alhaj Mbaraka Batenga ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Chunya, aliagiza viongozi wote wa serikali za mitaa katika mkoa huo kuhakikisha wanawafahamu wananchi wote wanaoishi kwenye maeneo yao.

Aliwataka kuwaorodhesha kwenye madaftari maalum pamoja na shughuli wanazofanya ili kuzuia uhalifu kwenye maeneo yao pamoja na maeneo jirani.


Victoria FINANCE

Victoria Finance Plc
5th Floor, Mwanga Tower Building-Kijitonyama
NewBagamoyo Road
P.O.Box 12102, Dar es Salaam - Tanzania
Telephone +255 22 277 4577
Fax: +255 22 277 4559
Email: info@victoriafinance.co.tz
Website: www.victoriafinance.co.tz

## TANGAZO LA MINADA YA HADHARA

VICTORIA FINANCE PLC INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| NA. | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | NYARAKA YA UMILIKI | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | VERDIANA A. MASANJA | NYUMBA - MPIJI MAGOE | SALES AGREEMENT | LEHAREL GROUP OF COMPANY | 02/04/2024 |
| 2 | BERNARD C. KAZOBA | LORI LENYE KRENI | T901 BZD - MITSUBISHI CANTER | JODAC PROFESSIONAL CO. LTD | 02/04/2024 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika vyombo husika vya Serikali.

**MASHARTI YA MNADA;**

- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Gharama za kumuhamisha mmiliki na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
- Dhamana itauzwa Kama ilivyo.



## UBALOZI WA MAREKANI NA EU DAR ES SALAAM

## MNADA WA HADHARA:

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na Ubalozi wa Marekani na EU watauza kwa mnada wa hadhara Fanicha, Magari na Generator **tarehe 23 March, 2024 Jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi.** Mnada utafanyika Golden Resort Sinza, Lion Street.

Fanicha na Computer zitaanza kuuzwa kuanzia saa 4:00 asubuhi: Sofa set, Sofa bed, Chest drawer, Meza za chakula na Viti, Book case, Dresser, Meza za ofisi na Viti, Steel cabinets, Vitanda, Magodoro, Fridge double door, UP Right freezer, Washer, Dryer m/c, Majiko ya umeme, Mashine za mazoezi (Tread Mill), Flat TV set, Laptop, Computer sets, A/c split unit, safe, na vingine vingi.

**Magari na Genereta yataanza kuuzwa Saa 6:00 mchana**

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 2 | Ford Everest Station Wagon | 3.0 Diesel Engine | 2012 | Haujalipwa |
| 1 | Nissan Patrol Station Wagon | TD42 Diesel Engine | 2009 | Haujalipwa |
| 1 | Suzuki Grand Vitara Station Wagon | J20 Petrol Engine | 2006 | Umelipwa |
| 3 | John Deere Club Car 750Kgs. | Linatumia Umeme | 2018 | Haujalipwa |
| 1 | Generator 60 KVA - 3Phase | Perkins Diesel Engine | 2007 | Haujalipwa |
| 2 | Generators 500 KVA - 3 Phase | Perkins Diesel Engine | 2007 | Haujalipwa |
| 1 | Voltage Stabilizer | Digital | - | Haujalipwa |

Mali zote zinaweza kukaguliwa Golden Resort Sinza,Lion Street kuanzia tarehe 20 mpaka 22 March 2024, kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni.

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi wa Fanicha atatakiwa kulipa malipo yote kwa keshia (cashier). Na mnunuzi wa Gari au Generator atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 5 za kazi mwisho wa kulipa tarehe 30 March, 2024 Saa 10:00 jioni. Ukishindwa kulipa kwa muda huo Gari au Genereta litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Malipo kwa njia ya VISA na Master cards za CRDB na NBC yanakubalika.
3. Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.
4. Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.
5. Mali yote iliyouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi
6. Kila mtu atatakiwa lazima kuwa na bid namba itakayopatikana getini na kuvaa barakoa.

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE DAR ES SALAAM**
**PLOT NO: 5 "E" LION STREET SINZA**
**CELL NO: 0754 284 926**
**E-mail: universalauction@hotmail.com**
**Insta: universalauctioncentre**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wateule wanapaswa kuzingatia kuhusu utekelezaji wa majukumu

**WIKI** iliyopita, Rais Samia Suluhu Hassan alifanya uteuzi na utenguzi wa viongozi katika ngazi mbalimbali, lengo kuu likiwa kuimarisha utendaji kazi serikalini kama ambavyo amekuwa akisema mara kwa mara anapofanya hivyo.

Kazi hiyo aliifanya mara tatu ndani ya wiki moja huku baadhi ya wateule hao wakiwekwa benchi na wengine kupandishwa ngazi na kubadilishwa majukumu au vituo vya kazi. Baada ya kumaliza hilo, hatua iliyofuata ilikuwa kuwaapisha wateule na kula kiapo cha maadili.

Katika hafla ya kuwapisha wateule hao iliyofanyika Ikulu, jijini Dar es Salaam, Rais Samia alizungumza mambo mbalimbali yanayohusu changamoto za watendaji ama aliowahamisha au kuwaondoa katika nafasi zao. Kwa wale waliobadilishiwa majukumu pia aliwapa maagizo kuhusu nini kinachowapasa kutenda na pia alitaja changamoto ya kila eneo walikopelekwa wateule hao.

Miongoni mwa mambo aliyoyazungumza kwa wateule hao ni pamoja na kuyajua vyema maeneo waliyopangiwa kwenda kufanya kazi, kutokuelewana baina ya wateule hao na baadhi ya watendaji, kutumia mabavu katika kusimamia mambo na kuzorota kwa utendaji kazi kwa baadhi yao.

Rais alibainisha kuwa Mkuu mpya wa Mkoa wa Songwe, Daniel Chongolo, anaufahamu vyema mkoa huo tangu alipokuwa Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), hivyo ana imani atakwenda kutatua changamoto mbalimbali ndani ya eneo hilo. Sambamba na hilo, alimtuma kwenda kushughulikia suala la biashara katika mji wa Tunduma ambao ni chanzo kikubwa cha mapato katika mkoa lakini kuna ukwepaji mkubwa wa kodi na biashara za magendo.

Licha ya kusema hayo, kuna jambo ambalo Rais Samia alizungumzia kwa undani wateule wengi kutokuwajibika ipasavyo ikiwamo kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kutatua kero zinazowakabili wananchi. Kwa ujumla, hilo ni suala ambalo huenda amekuwa akikerwa nao na hata kufikia hatua ya kufanya mabadiliko ya mara kwa mara kwa kuteua watu wapya na wengine uteuzi wao kutenguliwa.

Bila kuuma maneno wala kupepesa macho, Rais Samia aliwakumbusha kwamba wakuu wa mikoa ni wawakilishi wa Rais katika maeneo husika lakini bado kuna kero mbalimbali kwenye sehemu hizo na hazitatuliwi mpaka viongozi wa ngazi za juu serikalini wanapokwenda huko. Pia alisema katika ngazi ya mkoa kuna wilaya ambako wakuu wake wanaapishwa na wakuu wa mikoa lakini nao hawatimizi wajibu wao kama inavyotakiwa.


Kwa kauli hizo pekee, inaonyesha dhahiri kwamba katika maeneo hayo ya utawala kuna matatizo makubwa ama kwa viongozi waliopewa dhamana ya kuyaongoza kutokujua wajibu wao au kufanya kazi kwa mazoea. Kauli aliyoitoa Rais Samia inawapasa wateule hao katika mikoa, wilaya na serikali na taasisi zake kuamka na kuanza kufanya kazi kulingana na majukumu yao.

Jambo la kujiuliza inakuwaje mkuu wa mkoa ambaye ana watendaji katika kila sekta wakiongozwa na katibu tawala kushindwa kutimiza wajibu wao? Wanayatambua majukumu yao barabara au wako katika nafasi hizo bila kujitambua kwamba wanapaswa kufanya nini?

Mara nyingi imeshuhudiwa viongozi wa kitaifa kama Rais, makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Naibu Waziri Mkuu pamoja na viongozi wakuu wa CCM wanapotembelea maeneo mbalimbali ndipo matatizo kama ukosefu wa maji, ulanguzi wa mbolea, ubadhirifu wa fedha na mali za umma na migogoro ya ardhi yanaibuliwa huku wakuu wa mikoa na wilaya wakiwa wapo. Huu ni udhaifu wa hali ya juu kwa wateule hao na kwa ujumla, anachofanya Rais kuwaweka kando baadhi anastahili sifa.

Kama alivyosema Rais na kutoa maagizo kwa wateule hao, ni vyema sasa wakajitambua kuwa wanapaswa kufanya nini na kuanza kutekeleza wajibu wao kwa mujibu wa maelekezo na majukumu yao. Kama hawatafanya hivyo, wa wazi kwamba siku si nyingi nao watatenguliwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Halfani Chusi

## Muungwana Lazima Nilonge

# Rehema apewe maua yake, siku yao awa na kinamama gerezani Segerea

**UKISIKIA** kubeba agenda ya kuwainua wanawake ndio huku sasa, wanawake waishio Wilaya ya Ilala wako mikono salama kuwezeshwa kiuchumi na hata kupewa elimu ya ujasiriamali.

Msukani wa yote hayo, ni Mwenyekiti wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Rehema Sanga.

Kwa wanawake wa wilaya ya Ilala jina lake sio geni masikioni mwao. Hiyo ni kutokana na ukubwa wa mambo anayoyafanya katika jamii yanayowabeba zaidi wanawake.

Lililonikuna kwake zaidi, kusikia akisema Siku ya Wanawake Duniani, aliamua kusherehekea kwa kuwatembelea wafungwa wanawake walioko katika Gereza la Mahabusu Segerea na baadaye akaenda kutoa msaada katika Hospitali ya Bonyokwa, kusaidia ukamilishaji wa wodi ya kujifungulia kinamama.

Rehema anasema, katika kutekeleza hayo, alishirikiana na viongozi kutoka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Ilala, Idara ya Maendeleo Jamii Halmashauri ya jiji la Dar es Salaam.

"katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, mara nyingi tumekuwa 'tunakula bata', lakini safari hii tukasema tuwakumbuke wanawake waliopo katika Gereza la Segerea kwa kuwapatia msaada wa mahitaji mbalimbali.

"kilichonishangaza zaidi, tumekuta mikoba mizuri ya baadhi ya wanawake waliokuwa kwenye hilo gereza, kuna 'programu' ya mafunzo inaendeshwa nimehamasika kwa kuona kuna wanawake wanazalisha bidhaa huko upande wa pili.

"Nikaona tunaweza kuwasaidia kukuza soko la bidhaa zao ikawasaidia kupata fedha kwa ajili ya uendeshaji, ndio maana tuliguswa tukaona twende huko," anasema Rehema.

> **"katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, mara nyingi tumekuwa 'tunakula bata', lakini safari hii tukasema tuwakumbuke wanawake waliopo katika Gereza la Segerea kwa kuwapatia msaada wa mahitaji mbalimbali.**

Mwanamkwe huyo anawashauri wadau wengine wa maendeleo, waendelea kuwakumbuka wanawake walioko gerezani ili waweze kupata mahitaji muhimu.

Anaisema anatamani wadau waguswe wapeleke vitu kama magodoro, sabuni za kuogea, kufulia na kuwasapoti kwa kununua bidhaa wanazozalisha ili wapate kipato.

"Sisi kama Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, tutahakikisha bidhaa zao zinafika sokoni, pia zipate majina na wadau wazinunue kwa lengo la kusapoti miradi ya wanawake walioko gerezani. Tunaamini wakimaliza vifungo vyao watautumia huo ujuzi kwa nia ya kujiendeleza.

"Wana miradi mingi ya bustani, kushona kwa hiyo tunaangalia namna gani tutawasaidia bidhaa zao kutoka nje zikauzwa," anasema Rehema.

Ni simulizi kwamba, akaongozana na kutoa msaada huo zahanati ya Bonyokwa aliongozana na Mbunge wa Jimbo la Segerea, Bonnah Kamoli kutoa msaada wa kifedha kurekebisha wodi ya kujifungulia kinamama na kuepeleka vifaa vyake.

Ni aina ya misaada ambayo jamii inapaswa kutoa, kuwakumbuka wenye uhitaji maalumu kama watoto yatima, wajane, kama ambavyo Jukwaa la Uwezeshaji Kiuchumi Halamashauri ya Jiji la Ilala limethubutu.

Ni jambo lililoukosha uongozi wa hospitali na wana - Bonyokwa kwa ujumla kwamba msaada huo utasaidia kuboresha upatikanaji wa huduma ya afya kwa mjamzito.

# Wanawake Malawi walivyofanyiwa ukatili Oman walazimishwa kushiriki ngono bila ridhaa

**LILONGWE,** MALAWI

UMASKINI wa baadhi ya maeneo ikiwamo Malawi umekuwa sababu ya wanawake kushawishika kwenda kufanya kazi katika mataifa mengine kama Oman ili kujikwamua kimaisha, licha ya kwamba wengi wao baada ya kufika hujikuta wakidumbukia kwenye janga la kufanyiwa ukatili tofauti na matarajio.

Mwanamke mwenye umri wa miaka 32 anaangua kilio anapokumbuka unyanyasaji alioupata wakati akitarajia maisha mazuri, ambaye alijikuta akifanya kazi za ndani nchini Oman.

Mwanamke huyo aliyetambulishwa kwa jina moja Georgina, na wanawake wengine 50 waliosafirishwa kwa njia haramu, anaeleza kuwa aliamini ameajiriwa kufanya kazi ya udereva huko Dubai, jambo ambalo halikuwa hivyo.

Anasema alikuwa akifanya biashara ndogo ndogo mjini Lilongwe nchini Malawi, ndipo alipofuatwa na wakala na kumshawishi kwamba atapata pesa nyingi zaidi endapo akikubali kwenda kufanya kazi Oman.

Anasema baada ya kukubali na kusafiri, baada ya kufika Muscat, mji mkuu wa Oman, ndipo alipogundua amedanganywa na hatimaye kuingia katika familia ambayo ilimfanya afanye kazi kwa saa nyingi, siku saba kwa wiki.

**TAKWIMU**

Inakadiriwa kuwa kuna wafanyakazi wa nyumbani takribani milioni mbili katika mataifa ya Ghuba ya Kiarabu.

Katika uchunguzi wa wanawake 400 nchini Oman uliofanywa na shirika la misaada la wahamiaji la Do Bold, uliochapishwa 2023, ukisema karibu wote walikuwa wahanga wa biashara haramu ya binadamu.

Aidha, takribani theluthi moja wanasema walinyanyaswa kingono, huku nusu wakiripoti unyanyasaji wa kimwili na ubaguzi.

Georgina, anasema baada ya wiki kadhaa, alikata tamaa na akaweka chapisho kwenye Facebook kuomba mtu amsaidie.

Mwanaharakati wa mtandao wa kijamii wa Malawi, Pililani Nyoni, aliona ujumbe wa binti hiyo na kuanza kuchunguza.

Inaelezwa kuwa alifanya mawasiliano na ujumbe huo ukaondolewa Facebook kwa usalama wa Georgina na kuweka namba yake ya WhatsApp ambayo ilianza kusambaa nchini Oman. Ndipo aligundua tatizo ni kubwa.

Anabainisha kuwa zaidi ya wanawake 50 wa Malawi wanaofanya kazi kama wafanyakazi wa nyumbani nchini Oman walijiunga na kikundi hicho.

Inabainishwa kuwa punde kundi hilo la WhatsApp lilijaa sauti na video, zingine zikiwa za kuhuzunisha sana kutazama, zikielezea hali ya kutisha ambayo wanawake hao walikuwa wakipitia. Wengi wao pasipoti zao zikiwa zimechukuliwa mara tu walipofika, na kuzuiwa kuondoka.

Inaelezwa kuwa wengine walisimulia jinsi walivyojifungia kwenye vyoo ili kutuma jumbe zao kwa siri na jumbe za kuomba msaada.

Nyoni anasema alianza kuzungumza na mashirika nchini Malawi na akatambulishwa kwa Ekaterina Sivolobova, mwanzilishi wa Do Bold, iliyoko Ugiriki.

Do Bold ni shirika linalofanya kazi na jumuiya ya wafanyakazi wahamiaji katika nchi za Ghuba, kuwatambua waathiriwa wa biashara haramu ya binadamu au kazi za kulazimishwa na kisha kujadiliana na mwajiri wao ili waachiliwe.

Pia anaeleza kuwa mtindo huo unajulikana Mashariki ya Kati kama mfumo wa kazi wa kafara ambao wafanyakazi na waajiri wao huwa wote kwa muda wote wa mkataba.

Kamati ya Kitaifa ya Oman ya Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu iliiambia BBC kwamba mkataba kati ya mwajiri na mfanyakazi wa ndani ni wa makubaliano ya pande mbili na mizozo kati yao inaweza kuwasilishwa katika mahakama ndani ya wiki moja. **BBC**

# Adaiwa kuua mtalaka kwa panga kisha kujinyonga

**Na Julieth Mkireri,** KISARAWE

DOTTO Magambazi (30), mkazi wa Mtaa wa Mjimwema, Kata ya Kiluvya, wilayani Kisarawe, mkoani Pwani amefariki dunia baada ya kushambuliwa kwa kukatwa mapanga na anayedaiwa mtalaka wake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP), Pius Lutumo aliwaeleza waandishi wa habari jana ofisini kwake kwamba Dotto alifariki dunia akiwa anapatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Pwani (Tumbi).

Kwa mujibu wa Kamanda Lutumo, Dotto alishambuliwa kwa panga maeneo mbalimbali ya mwili wake saa tatu usiku Machi 17, mwaka huu na alifariki dunia saa tano usiku.

Alisema uchunguzi wa awali uliofanywa na Jeshi la Polisi umebaini aliyehusika na shambulio hilo ni aliyekuwa mume wake, Mbaraka Mapunda (42), mkazi wa Chanika, Dar es Salam aliyetalikiana naye mwaka mmoja uliopita.

Chanzo cha shambulio hilo kinadaiwa ni wivu wa mapenzi na kugombea mali walizochuma pamoja.

Hata hivyo, wakati jeshi hilo likiendelea na msako kumkamata mtuhumiwa, ilibainika baadaye amefariki dunia kwa kujinyonga kwenye kichaka umbali wa mita 300 kutoka nyumbani Mtaa wa Mjimwema.

Mtuhumiwa huyo anadaiwa kujinyonga kwa kutumia mkanda wa nguo ambao aliutumia kujining'iniza kwenye mti.

# HESLB, ZEEA waingia makubaliano kuwatafutia fursa ajira wahitimu

**Na Beatrice Shayo**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imeingia makubaliano na Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar (ZEEA) kuendelea kutafuta fursa za ajira kwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu itakayowawezesha kurejesha.

HESLB inadai zaidi ya Sh. bilioni 700 kwa wanufaika wa mikopo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi baada ya utiaji saini makubaliano hayo, Mkurugenzi wa HESLB, Dk. Bill Kiwia, alisema watashirikiana kuandaa mazingira mafunzo ya kuongeza ujuzi katika sekta ya utalii sambamba na fursa za ajira.

Wakili Murusuri aliendelea kudai mahakamani kuwa ofisa ununuzi msaidizi na mzabuni walijipatia manufaa yasiyostahiki kwa ununuzi huo hewa na kwamba Sh. 2,800,000 zililipwa kwa mzabuni bila kupeleka vifaa husika.

Baada ya Wakili Kiongozi wa TAKUKURU kumaliza kuwasomea washtakiwa hao maelezo ya awali, Hakimu Mwambeleko aliwahoji washtakiwa hao, wote wakakiri makosa yao.

"Washtakiwa wote kwa pamoja mahakama hii imewatia hatiani kwa kosa mliloshtakiwa nalo, pia mahakama hii inawataka washtakiwa kutoa maombi yenu ili mahakamama hii iweze kuwapunguzia adhabu," alisema.


Washtakiwa wote kwa pamoja wakati wa maombi ya kupunguziwa adhabu, waliomba mahakama iwapunguzie adhabu kwa kuwa wana familia zinazowategemea.

Upande wa Mashtaka ukiongozwa na Wakili Kiongozi wa TAKUKURU Mkoa wa Kagera, Murusuri, uliomba mahakama iwape washtakiwa adhabu kali ili iwe fundisho kwao na maofisa ununuzi wengina pamoja na wazabuni wanaoendekeza vitendo vya rushwa katika ununuzi na kuitia hasara serikali.

Wakili Murusuri pia aliomba mahakama iwaamuru washtakiwa wote kwa pamoja kurejesha fedha Sh. 2,800,000 zilizolipwa kwa ununuzi hewa.

Hakimu Mwambeleko alisema amezingatia maombi ya pande zote mbili na kuwahukumu washtakiwa kutumikia kifungo cha miaka miwili jela au kulipa faini ya Sh. milioni moja, ili iwe fundisho kwa maofisa ununuzi na wazabuni wanaoendekeza vitendo vya rushwa katika ununuzi.

Hakimu Mwambeleko pia alisema ameridhia maombi ya upande wa Jamhuri ya kutaka fedha Sh. 2,800,000 zilizokuwa zimelipwa pasipo ununuzi zirejeshwe na kukabidhiwa katika Ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Muleba.



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM (AT KINONDONI)

CRIMINAL CASE NO. ......137.............OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

GODFREY SERERYA.........................................ACCUSED PERSON

To:
Godfrey Sererya
Kifurukwe Street, Kibada Area,
Kigamboni Municipality
**Dar Es Salaam Region**

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT, CAP. 235 OF THE LAWS AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 4TH day of APRIL 2024 at **08:00 am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**


GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 29 day of FEBRUARY 2024

RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE KINONDONI DISTRICT COURT DAR ES SALAAM

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me/us:**
Name.............................
Signature.............................
Qualification/Relationship
Date.............................



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM (AT KINONDONI)

CRIMINAL CASE NO. ..134.... OF 2023.

THE REPUBLIC

VERSUS

BERNARD KIREI.........................................ACCUSED PERSON

To:
Bernard Kirei,
Plot No. 2037, Block A, Tip Top Street, Manzese Area
Kinondoni Municipality
**Dar Es Salaam**

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 4TH day of APRIL 2024 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 29 day of FEBRUARY 2024

RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE KINONDONI DISTRICT COURT DAR ES SALAAM

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me/us:**
Name.............................
Signature.............................
Qualification/Relationship
Date.............................



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM (AT KINONDONI)

CRIMINAL CASE NO. 133... OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

ADATUS KAPES.........................................ACCUSED PERSON

To:
Adatus Kapes,
Plot No. 3, Block A, Mbezi Area
Kinondoni Municipality
**Dar Es Salaam**

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 4TH day of APRIL 2024 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**


GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 25TH day of FEBRUARY 2024

RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE KINONDONI DISTRICT COURT DAR ES SALAAM

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me/us:**
Name.............................
Signature.............................
Qualification/Relationship
Date.............................



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM (AT KINONDONI)

CRIMINAL CASE NO. 138.... OF 2023.

THE REPUBLIC

VERSUS

WEMAELI ELIAMANI MSUYA.........................................ACCUSED PERSON

To:
Wemaeli Eliamani Msuya,
Kwa Mchigani Area, Goba Ward
Ubungo Municipality
**Dar Es Salaam**

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 4TH day of APRIL 2024 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 29 day of FEBRUARY 2024

RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE KINONDONI DISTRICT COURT DAR ES SALAAM

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me/us:**
Name.............................
Signature.............................
Qualification/Relationship
Date.............................

# CRDB yawapa msaada watoto wanaoishi mazingira magumu

**Na Mwandishi Wetu**

IKIUNGANA na jumuiya ya Waislamu nchini katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhan, Benki ya CRDB imetoa msaada wa vyakula na mahitaji mengine muhimu kwa vituo vya kulea watoto wenye mahitaji maalum.

Msaada huo uliotolewa jana baada ya Swala ya Magharibi na futari iliyoandaliwa katika Hoteli ya Johari Rotana, jijini ikiwashirikisha wateja, wabia, menejimenti na wadau wengine muhimu. Ulipokewa na kituo cha kulea watoto cha Masjid Suleiman kilichoko wilayani Kigamboni na Masjid Aqswaa kilichoko Mbezi Luis, wilayani Ubungo.

Akiwasalimia wageni waalikwa, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela alisema Mwezi Mtukufu wa Ramadhan ni kipindi cha kujumuika na familia, ndugu na jamaa katika futari, ndio maana benki anayoiongoza imejiwekea utamaduni kuandaa futari maalum kwa ajili ya wateja na wadau wengine ili kudumisha nguzo hiyo ya Uislamu inayomjenga mja kuwa mtiifu, mwenye subira na tabia njema kwa muumba na binadamu wengine.

"Katika futari hizi, tumekuwa tukiungana na wenzetu waliopo katika mazingira magumu. Hii ni kwa kutambua kuwa Mwezi wa Ramadhan huambatana na kutoa sadaka au kuwasaidia wasiojiweza. "Pamoja na futari hii tuliyoiandaa kwa ajili ya wateja na wadau wetu, benki yetu imeona ni jambo la faraja kutoa sadaka kwa vituo vya watu wenye mahitaji maalum," alisema Nsekela kabla ya kukabidhi mchele, unga, sukari, maharage, tambi, tende, mafuta, maziwa, majani ya chai na sabuni kwa kila kituo.

Vilevile, Nsekela aliitumia fursa hiyo kuelezea Benki ya CRDB inavyobuni bidhaa na huduma zinazokidhi mahitaji ya Waislamu pamoja na Watanzania wote kwa ujumla kwa kujali imani yao, akizitaja CRDB Al Barakah na Takaful.

Kuhusu Takaful, alisema ni bima yenye misingi ya sheria kuwasaidia wateja kuzikinga mali na biashara zao kwa kuendana na imani zao. Huduma zote mbili, yaani CRDB Al Barakah na Takaful, alisema zinatolewa kwenye matawi yote zaidi ya 260 ya Benki ya CRDB nchini.

"Benki yetu imeanzisha huduma zinazofuata misingi ya sheria ili kuwajumuisha Watanzania wengi katika huduma za fedha bila kuathiri imani zao.


"CRDB Al Barakah ni akaunti inayowezesha makundi mbalimbali ya wateja safari ya ibada ya Hajj na Umrah. Tangu kuanzishwa kwake mwaka 2021, tayari imewajumuisha zaidi ya Watanzania 150,000 na kutoa mikopo yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 135," alisema Nsekela.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na Sheikh Aboubakar Bin Ali Zuberi, Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania ambaye alikuwa mgeni rasmi akiwakilishwa na Naibu Kadhi na Kaimu Mufti wa Tanzania, Sheikh Ally Khamis Ngeruko, aliyesema Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ni kipindi muhimu kwa Waislamu kujisogeza karibu na muumba wao.

"Maisha yetu wanadamu hapa duniani ni mafupi sana. Tuna kila sababu ya kutenda mema yampendezayo Mwenyezi Mungu kwa wanadamu wenzetu.

"Mola wetu anapenda kutuona tukishirikiana na kupendana. Tufanye haya kwa ajili ya baadaye yetu pindi tutakapoiacha dunia," alisema Sheikh Ngeruko.

Kaimu Mufti huyo aliongeza: "Ninawapongeza pia Benki ya CRDB kwa kubuni huduma zinazofuata misingi na sheria kwani hii si tu itaongezeka ujumuishi wa kifedha katika jamii hasa waumini wa dini



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO. 222 OF 2023.

THE REPUBLIC

VERSUS

ROBERT MARTIN KISANGA……………………1ST ACCUSED PERSON
OTHMAN MUSHI……………………………2ND ACCUSED PERSON

To:
Robert Martin Kisanga & Othman Mushi
Pugu Kajiungeni Area
Ilala Municipality
Dar Es Salaam City

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on Engaging unregistered person or firm to undertake construction works, Contrary to *Section 22(4)* of the *Contractors Registration Act No. 17 of 1997* as amended by *Section 20* of *Contractors Registration (Amendments) Act No. 15 of 2008.*

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 4TH day of APRIL 2024 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.


Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 29TH day of FEBRUARY, 2024

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:
Name……………………
Signature……………………
Qualification/Relationship
Date……………………



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO. 15 OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

OMARY MUHINDI MATAKA……………………ACCUSED PERSON

To:
Omary Muhindi Mataka
Plot No. 317, Mikocheni Area
Kinondoni Municipality
Dar Es Salaam

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 4TH day of APRIL 2024 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.


Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 29TH day of FEBRUARY 2024

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:
Name……………………
Signature……………………
Qualification/Relationship
Date……………………



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO. 129 OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

LUSUBILO MWAKABIBI……………………ACCUSED PERSON

To:
Lusubilo Mwakabibi
Kijitonyama Area,
Kinondoni Municipality, Dar Es Salaam

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 4TH day of MARCH 2024 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.


Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 29TH Day of FEBRUARY, 2024

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:
Name……………………
Signature……………………
Qualification/Relationship
Date……………………



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO. 130 OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

NASSOR FILING STATION CO. LIMITED……………………ACCUSED PERSON

To:
Nassor Suleiman Nassor
Director / shareholder
Nassor Filing Station Company Limited
Plots Nos. 714, 715 & 716, Block B, Pugu Mwakanga Area
**Dar Es Salaam Region**

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT, CAP. 235 OF THE LAWS AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 4TH day of APRIL 2024 at 08:00 am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 29TH day of FEBRUARY 2024

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:
Name……………………
Signature……………………
Qualification/Relationship
Date……………………



## RC apiga marufuku ukodishaji wa mashamba ya shule

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

MKUU wa Wilaya ya Mkalama mkoani Singida, Moses Machali, amepiga marufuku ukodishaji wa mashamba ya shule na kuagiza yatumike kuzalisha chakula kwa ajili ya wanafunzi.

Alipiga marufuku hiyo jana wakati akizungumza na wananchi wa vijiji vya Asanja na Mwanga kwenye mikutano ya hadhara ya kusikiliza na kutatua kero zinazowakabili wananchi wa vijiji hivyo.

"Marufuku kukodisha mashamba ya shule, mashamba ya shule yatumike kwa ajili ya kuzalisha chakula kwa wanafunzi. Nisisikie mtu anakodisha shamba la shule wala msiuze ardhi ya serikali bila sababu, msipokuwa makini mtakuja kufanywa manamba hapa," alisema.

Machali alisema mashamba ya shule yakitumika kwa ajili ya kuzalisha mazao kutasaidia wazazi kuwapunguzia mzigo wa kuchangia chakula kwa ajili ya watoto wao wanaosoma katika shule husika.

Aidha, alipiga marufuku wananchi kuuza mazao yakiwa bado shambani kwa kuwa utaratibu huo ambao unafanywa na baadhi ya wafanyabiashara unawanyonya wakulima wasiweze kunufaika na kilimo kutokana na mazao yao kununuliwa kwa bei ndogo mashambani.

Alisema kuna tabia kwa baadhi ya wafugaji kupeleka mifugo yao katika mashamba ya watu na kusababisha migogoro kati ya wakulima na wafugaji na kwamba atakayebainika atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Akijibu swali kuhusu suala la maji safi na huduma ya umeme katika vijiji vya Asanja na Mwanga, aliwaeleza wananchi kuwa serikali tayari imeweka mpango wa kupeleka huduma hizo kwenye vijiji hivyo.

# Utafiti: Asilimia 53 ya watoto wako hatarini ukuaji ubongo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MATOKEO ya Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mwaka 2023, umebaini kuwa asilimia 53 ya watoto nchini wenye umri wa miaka miwili hadi mitano wako katika hatari ya kutofikia kiwango cha ukuaji wa ubongo.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Amon Mpanju, alitoa kauli hiyo jana jijini hapa kwenye kikao kazi cha uwasilishaji wa Viashiria vya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto kwa Mwaka 2030.

Alisema matokeo ya utafiti huo yanaonesha kuwa asilimia 47 ya watoto walio katika umri huo ndiyo wenye mwelekeo sahihi wa makuzi, malezi na maendeleo ya awali ya mtoto.

Mpanju, alisema hali hiyo ni hatari kwa taifa kama hatua za haraka hazitachukuliwa ili kuwa na rasilimali watu ambayo itaweza kujisimamia yenyewe pamoja na taifa.

"Eneo hili la makuzi, malezi na maendeleo ya awali ya mtoto ni eneo nyeti sana kwa taifa letu, leo hii tunaweza tukawa tunawekeza katika vitu kama ardhi, barabara lakini kama tutakuwa taifa ambalo halina watu ambao wako timamu kichwani itakuwa shida," alisema Mpanju.

Alisema suala la malezi na makuzi ni mtambuka, hivyo kila mtu anawajibu wa kuhakikisha taifa linakuwa na kizazi ambacho kitakuwa kinajitambua ili kuweza kusimamia rasilimali zao.

Aidha, alizitaka halmashauri zote nchini kutenga bajeti ambazo zitasaidia kuwezesha malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto katika maeneo yao.

"Kama hatutachukua hatua tunaweza kuwakosa marais wa badaye, madaktari lakini raia wema ambao watakuwa tayari kulitumikia taifa lao na kulinda rasilimali zilizopo nchini."

"Pia tunaweza kuwa na kizazi cha ajabu ambacho hata hakina uwezo wa kusimamia rasilimali zao kama hatuta wekeza kwenye malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto," alisisitiza Mpanju.

Meneja wa Takwimu za Jamii kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Sylvia Meku, alisema utafiti zinaonyesha moja kati ya sababu ya malezi na makuzi duni ni elimu kwa wazazi na walezi.

"Utafiti zinaonyesha kuwa wazazi ambao kidogo wamepata elimu suala la malezi na makuzi kidogo mwelekeo upo lakini ambao hawana elimu kuna shida lakini pia uchumi umeonekana ni tatizo katika familia," alisema.

Alisema athari za kutokuwa na malezi na makuzi bora ni pamoja na mmomonyoko wa maadili, uzalishaji duni ambao unaweza kusababisha taifa kushuka kiuchumi.

Meneja Mradi wa Mtandao wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto, Lazaro Ernest, alisema sayansi ya malezi inaeleza kuwa umri wa mwaka sifuri hadi miaka nane ndiyo kipindi sahihi cha kuwekeza katika malezi na makuzi ya mtoto.

Hata hivyo, alisema katika kipindi hicho ndipo ubongo wa mtoto unakuwa kwa kasi, hivyo ni wakati muhimu kuwekeza katika malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto.



Diwani wa Kata ya Kizota, jijini Dodoma, Jamal Ngalya (kulia), akisikiliza kero mbalimbali za wananchi zinazohusu migogoro ya ardhi, juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Kanisa lajenga kituo cha polisi kuzuia uhalifu

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

KATIKA kukabiliana na tatizo la uhalifu wilayani Chamwino mkoani Dodoma, Kanisa la Faith in Christ International Ministries (FACIM) limesaidia ujenzi wa kituo cha polisi uliogharimu kiasi cha Sh. milioni 70.

Kituo hicho ambacho kimejengwa katika Kata ya Mlowa barabarani wilayani hapa, kwa gharama ya zaidi ya Sh. milioni 70 kitahudumia wakazi wa eneo hilo na vijiji jirani.

Katibu Mkuu wa Kanisa hilo Taifa, Mchungaji Christomus Kilapilo, akizungumza kwa niaba ya Askofu Mkuu, Gescker Matonya, alisema kuwa lengo la kujenga kituo hicho ni kuisaidia serikali kupambana na uhalifu kwenye eneo hilo.

Katibu huyo alisema pamoja na kanisa kuhakikisha inashughulika na roho za watu lakini pia limeona ipo haja kwao kusaidia serikali kukabiliana na tatizo la uhalifu wilayani hapo.

"Sisi kama kanisa kazi yetu ni kuhakikisha tunashughulika na roho za watu ili waache matendo maovu lakini ikumbukwe kuwa na serikali nao wanafanya kazi kuhakikisha wanalinda amani na mali za watu, hivyo ni matumaini yetu tukishirikiana kwa pamoja tutaondoa changamoto ya kutokuwapo na matendo mbalimbali ya kihalifu," alisema.

Kadhalika, alisema pamoja na ujenzi wa kituo hicho ambacho kitakabidhiwa mapema Aprili mwaka huu, malengo mengine waliyojiwekea kuifikia jamii ni pamoja na kusaidia serikali kwenye sekta ya elimu na huduma za afya. "Tumekijenga kituo hicho cha polisi lakini kwa upande wetu pia tunatarajia kujenga majengo ya makao makuu ya kanisa ikiwamo na ofisi zake pamoja na majengo yatakayosaidia jamii kama vile kituo cha afya na majengo ya shule za awali," alisema.

Awali akihubiri kwenye ibada ya kuwasimika viongozi na kuwaweka wakfu wachungaji, Mkuu wa Kanisa hilo aliwataka waliosimikwa kuifanya kazi zao kwa malengo ya kulitumikia kanisa na serikali.

Pia aliwataka kwenye huduma zao kukemea maovu ikiwamo ukatili wa kijinsia kwa lengo la kuisaidia serikali ili nchi ipate kizazi kitakachoaminiwa na jamii.

Pia, aliwataka kufanya kazi kwa kushirikiana kwa pamoja na washirika watakaowaongoza, ili kazi zao ziweze kuleta mafanikio yatakayowezesha kukuza uchumi kwa kanisa na serikali.

Waliosimikwa na kuwaweka wakfu ni pamoja na Makamu Askofu Mkuu, George Paul, Katibu Mkuu, Mhasibu Mkuu wa Kanisa, Mshauri Mkuu, Katibu Ofisi ya Makamu wa Askofu.

Wengine ni maaskofu wa majimbo, makatibu wa majimbo, wahasibu wa majimbo, wakurugenzi, makatibu wa idara na wachungaji wa makanisa.





# Jamii yaonywa kuficha watoto wenye ulemavu

**Na Elizabeth John,**
WANGING'OMBE

JAMII mkoani Njombe imetakiwa kuachana na imani potofu kwa watoto mwenye ulemavu wa viungo kwa kuamini kwamba limetokana na kurogwa na kukimbilia kwa waganga wa kienyeji badala yake wawapeleke kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Kauli hiyo imetolewa na Mkuu wa Hospitali ya Inuka, wilayani Wanging'ombe mkoani Njombe, Padre Nestory Mtweve, kwa viongozi wakuu na walezi wa kwaya ya Mtakatifu Mbaga Tuzinde ya Kanisa Katoliki la Mtakatifu Yosefu, Jimbo la Njombe walipokwenda kukabidhi msaada wa pampu ya kuvuta maji.

"Tafsiri potofu ya kuhusisha ulemavu na uchawi ni sehemu ya wanachokiamini watu wa maeneo haya," alisema Mtweve. Mtweve alisema mtoto anapopata tatizo la ulemavu wanaanzia kwa waganga wa kienyeji ikishindikana huamua kwenda hospitali.

"Kwa maana yake wanaanzia kwanza huko baadaye ndiyo wanaanza kuhangaika kwenda huku na huko hadi kufika hapa hospitali na ikifika siku moja mbili mtoto anaanza kuinua mkono," alisema Mtweve.

Awali, Mwenyekiti kamati ya maandalizi, George Kinyamagoha, alisema msaada huo ni kutokana na kwaya hiyo kuchangishana fedha ili kusaidia hospitali hiyo kuondoka na changamoto hiyo ya muda mrefu.

"Kama leo tumeweza kuleta pampu basi mwakani Mungu akitupa uhai au mwaka huu tufanye kitu kikubwa zaidi mara mbili au mara tatu ya mahitaji yao, kwa sababu pampu hii inakwenda kusaidia wagonjwa kukabiliana na changamoto ya maji," alisema Kinyamagoha.

Mwenyekiti wa walezi wa kwaya hiyo, Deo Mtewele, alisema watazidi kuhamasishana kwa sababu wagonjwa waliopo wanahitaji msaada wa watu wote bila kujali dini wala kabila.

Mmoja wa wakazi wa mjini Njombe, Angelah Mwangeni, akizungumza na Nipashe, alikemea tabia ya baadhi ya walezi na wazazi wa watoto wanaopatwa na changamoto ya ulemavu kuacha mara moja kukimbilia kwa waganga wa kienyeji ili kumtibu mtoto.

Alikemea pia wazazi wenye tabia ya kuficha watoto wenye ulemavu kwa kuwanyima fursa nyingi ikiwamo ya kupata elimu.



Balozi wa Umoja wa Ulaya (EU) nchini Tanzania, Christine Grau (kushoto), akiangalia teknolojia ya nishati safi ya kupikia zinazo wezeshwa na mradi wa CookFund uliofadhiliwa na EU, katika Kongamano la Wanawake ya Nishati Safi ya Kupikia lilioandaliwa na Wizara ya Nishati, jijini Dodoma hivi karibuni. Wa pili kulia ni Meneja wa Mradi wa Nishati na Mjumbe wa EU nchini, Massimiliano Pedretti na (wa pili kushoto) ni Mtaalamu wa Fedha na Meneja wa Mpango wa CookFund, Imanuel Muro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# PM: Majina ya mitaa, barabara yaandikwe Kiswahili

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

SERIKALI imeagiza majina ya mitaa, barabara na mabango yanayotoa elimu kuhusu mambo mbalimbali nchini kuandikwa kwa Kiswahili badala ya lugha za kigeni ili kuwasaidia wananchi kuelewa ujumbe unaolengwa.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alitoa agizo hilo juzi alipokuwa akifungua Kongamano la Idhaa za Kiswahili lililofanyika jijini hapa na kuwaagiza wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya zote nchini kusimamia utekelezaji.

Aidha, aliagiza dawa na vifaa tiba ambazo maelekezo yake yameandikwa kwa Kiingereza ama lugha nyingine yoyote ya kigeni ufafanuzi wake uandikwe kwa Kiswahili chini ili kuwasaidia Watanzania kuelewa.

"Inaweza ikatokea kwamba kuna bango ambalo limewekwa mahali likilenga kuwaelimisha Watanzania wote, lakini limeandikwa kwa lugha ya Kiingereza na kusababisha wasiojua lugha hiyo kutoelewa, sasa ili kurahisisha basi pale chini tafsiri yake iandikwe kwa Kiswahili," alisema Majaliwa.

Aliwataka pia waandishi wa habari na watangazaji nchini kutumia Kiswahili kwa ufasaha kupitia vyombo vya habari ili kusaidia kuisambaza lugha hiyo.

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, alisema mwaka huu serikali imemtunuku tuzo ya heshima Rais wa Awamu ya Pili, Hayati Ali Hassan Mwinyi kutokana na mchango alioutoa kwenye ukuzaji wa Kiswahili.

Alisema wakati wa uongozi wake, Hayati Mwinyi alikuwa anazungumza Kiswahili fasaha wakati wote na kukosoa wale wote waliokuwa wanatumia vibaya lugha hiyo ama kutumia misamiati isiyofaa.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, Patrick Mwalunenge, aliwapongeza wadau mbalimbali kwa kuendelea kukuza Kiswahili akisema kuwa ni sehemu ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya chama hicho tawala.

Alishauri serikali kuendelea kuwahamasisha vijana katika ngazi mbalimbali za elimu, kuthamini utamaduni wao ikiwamo kutumia Kiswahili kama utambulisho wao.

Alisema Kiswahili kinasaidia kuimarisha usalama wa nchi kwa kuwa Watanzania wote wanatumia lugha hiyo kutambuana na kuwatambua watu wengine.

Kongamano la Kiswahili linawaunganisha wadau mbalimbali wakiwamo viongozi wa vyombo vyote vya habari vinavyorusha matangazo yake kwa lugha ya Kiswahili kwa lengo la kuelimishana na kujadili kero mbalimbali zinazoibuka wakati wa kusambaza lugha hiyo.

## HJFMRI yatenga mil. 500/- kuwezesha wasichana kiuchumi

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

SHIRIKA linalopambana na Maambukizi vya Virusi vya Ukimwi (HJFMRI), limetenga Sh. milioni 500, mwaka huu, kwa ajili ya kuwezesha kiuchumi wasichana rika balehe na wanawake vijana katika mikoa ya Mbeya na Songwe ili kuwaepusha na vishawishi vinavyosababisha wapate maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi.

Mkurugenzi wa Shirika la HJFMRI nchini Tanzania, Sally Chalamila, aliyasema hayo juzi kwenye hafla ya kukabidhi vifaa vya kisasa vyenye thamani ya Sh. milioni 178 kwa ajili ya kuwawezesha kiuchumi wasichana rika balehe na wanawake vijana wanaoshiriki kwenye mradi wa 'dreams' unaotekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, mkoani Mbeya.

"Kupitia utaratibu wa kuwawezesha mabinti, HJFMRI imetoa vyerehani vya kisasa vya kushonea nguo 80, mashine maalum ya kudarizi nguo za kisasa (16), kunakishia nguo (8), kufuma kwa mkono (6), kukamua mafuta ya alizeti (1), kutengeneza sabuni (1), kutengeneza viatu viwandani (2), mashine ya kunakishia viatu (8), vifaa hivyo vina thamani ya Sh. milioni 178," alisema Sally.

Mtaalamu wa masuala ya kuzuia maambukizi ya virusi vya Ukimwi kutoka Idara ya Ulinzi ya Marekani ya WRAIR/DOD, Dk. Alick Kayange, alisema mafanikio katika mapambano dhidi ya Ukimwi katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kuwa ni mwitikio wa wananchi kutumia kikamilifu dawa za kufubaza makali ya virusi hivyo.

Alisema WRAIR/DOD kupitia miradi inayoisimamia itahakikisha hadi kufikia mwaka 2030 inafikia sifuri tatu kusiwe na maambukizi mapya ya VVU, vifo vitokanavyo na maambukizi hayo wala unyanyapaa na kubaguana.

"Jitihada zetu lazima tuzielekeze kwenye kutoa huduma kwa usawa, ukilenga makundi yaliyo katika hatari ya kupata maambukizi ikiwamo mabinti walio kwenye umri balehe na wanawake vijana, wakiwezeshwa kiuchumi, wanakuwa wamepunguziwa uwezekano wa kupata maambukizi," alisema Dk. Kayange.

Akikabidhi vifaa hivyo kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama, Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Jaffar Haniu alisema malengo ya mradi wa dreams ni kudhibiti maambukizi mapya ya VVU kwa kuwawezesha mabinti kuwa na kipato kinachoweza kustahimili vikwazo vya kimazingira vinavyosababisha kuingia kwenye hatari ya kupata Ukimwi.

Miongoni mwa wanufaika wa mradi wa dreams wilayani Kyela, Shan Fanuel, alisema umebadilisha maisha yake kwa kumjengea uwezo wa kujitambua, kuachana na tabia hatarishi na kufanya shughuli za ujasiriamali ambazo zinamsaidia kuendesha maisha yake.





## Matumizi ya gesi kupikia yanusuru uharibifu mazingira

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANAWAKE wa Mkoa wa Kusini Unguja wamesema, matumizi ya gesi kwa ajili ya kupikia yanasaidia kupunguza ukataji wa misitu na kupunguza uharibifu wa mazingira.

Wanawake hao walisema hayo wakati wakizungumza na waandishi wa habari kwa nyakati tofauti baada ya kutumia nishati ya gesi ambazo wamewezeshwa na taasisi ya Kuwawezesha Wanawake Kielimu na kiuchumi Zanzibar (FAWE).

Walisema hatua hiyo inasaidia kwa kiasi kikubwa kuhifadhi mazingira kutokana na kuacha matumizi ya kuni.

Sichana Elekea Abdalla kutoka kijiji cha Uroa, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja, alisema kutokana na kutumia nishati ya gesi wameacha kukata miti kwa ajili ya kuni kwa matumizi ya kupikia.

Alisema awali walishindwa kufanya kazi zao kutokana na kutumia muda mwingi kwa ajili ya kutafuta kuni za kupikia, lakini baada ya kutumia gesi wanapanga mipango yao vizuri ya kuendeleza kazi zao ikiwamo ya ukulima wa mwani na kufanya shughuli nyingine za ujasiriamali ili kujikwamua kiuchumi.

Mkazi wa Makunduchi, Wilaya ya Kusini, Mkoa wa Kusini Unguja, Mtumwa Ame Vuai, alisema kutokana na umuhimu wa kutumia nishati hiyo wana mpango wa kufungua uwakala wa uuzaji wa gesi ili kuepusha usumbufu wa kuchukua muda mrefu baada ya gesi kumaliza na kurudia katika matumizi ya awali ya kuni.

Aidha, waliipongeza FAWE kwa kuwasogeza katika teknolojia ya kisasa ya kutumia gesi kwa ajili ya matumizi ya kupikia.

Mjumbe wa Bodi ya FAWE Zanzibar, Sabrina Omar Abdallah, alisema taasisi hiyo imeandaa utaratibu wa kuwasaidia wanawake wanaoishi maeneo mbalimbali wakiwamo wa Mkoa wa Kusini Unguja, mitungi ya gesi ya kupikia ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa.

Alisema lengo la kuwasaidia ni kuunga mkono jitihada za Serikali ya Zanzibar na Tanzania ya kupunguza matumizi ya kuni na mkaa ili kudhibiti mabadiliko ya tabianchi.

Alisema lengo lao ni kuhakikisha wanawake wanakuwa salama kutumia nishati ya kupikia pamoja na kurahisisha wakati wa kuandaa chakula ili kuendelea na harakati zao za kimaisha za ukuaji kiuchumi.

Aliwaomba wanawake waliopatiwa mitungi ya gesi itakapomalizika ni vyema kuendelea kuijaza na kuitumia ili kuwa mabalozi wazuri kwa wengine.

Kwa mujibu wa matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 hali ya utumiaji wa nishati ya kupikia Zanzibar inaonyesha asilimia kubwa ya wanakaya wanatumia kuni kwa ajili ya kupikia ukifuata mkaa ambao unatumika kwa asilimia 28.9 na nishati ya gesi ni asilimia 12.8 ikilinganishwa na sensa ya mwaka ya 2022.

Pia, matokeo ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 yanaonesha mikoa ya Kaskazini Pemba na Unguja na Kusini inatumia zaidi nishati ya kuni kwa asilimia 76.7 kwa ajili ya kupikia na kaya ya Mkoa Mjini Magharibi zinaongoza zaidi kwa kupikia mkaa kwa asilimia 48 na gesi asilimia 22.

# ‘Elimu itolewe kujua umuhimu wa misitu’

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIKA kuelekea maadhimisho ya kilele cha Siku ya Misitu Duniani inayoadhimishwa Machi 21 kila mwaka, jamii ishirikishwe katika utoaji wa elimu ili kujua umuhimu wa misitu.

Msaidizi Mkuu wa Hifadhi ya Kimaumbile ya Masingini, Amour Khamis Juma, alisema elimu hiyo itasiadia jamii kutambua rasilimali zilizopo ikiwamo wanyama, ndege na miti adimu na kuhifadhi mazingira.

Aliyasema hayo jana katika hifadhi ya kimaumbile ya Msitu wa Masingini nje ya mji wa Zanzibar, wakati akitoa elimu kwa wanafunzi wa Shule ya Mtoni Kigomeni na Mtopepo ‘B’ waliofika katika hifadhi hiyo. Amour alisema dunia huadhimisha siku hiyo ya misitu kwa lengo la kutunza mazingira ikiwamo kupanda miti, kutunza misitu, kuwapa hamasa wanajamii pamoja na kutunza mazingira kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Aidha, alisema maadhimisho hayo yalianza kuasisiwa na Shirika la Chakula Duniani (FAO), mwaka 2016 ikiwa na dhamira ya kuwaeleza wanajamii umuhimu wa utunzaji wa miti duniani.

“Wafanyakazi wa Idara ya Misitu tunaadhimisha siku hiyo kwa kupanda miti katika maeneo tofauti ya hifadhi, lakini kwa mwaka huu tutaadhimisha kwa kufanya mambo tofauti ikiwamo kuelimisha wanafunzi katika misitu yetu na hifadhi ya taifa ya Jozani,” alisema Amour.

Hata hivyo, alisema kuwa kilele cha maadhimisho hayo kitajumuisha shughuli za upandaji miti ya mikoko katika Hifadhi ya Taifa Jozani Shehia ya Charawe na kuzinduliwa mradi wa kitalii wa mnara wa Shehia ya Pete na ugawaji wa hundi kwa wadau wa hifadhi hiyo.

Mwalimu wa Shule ya Msingi Bububu ‘A’, Khatib Hamad Khatib, alisema wamehamasika na upewaji wa elimu kwa wataalamu wa misitu na kujua umuhimu wa kuhifadhi misitu na faida zake na elimu hiyo wataifikisha kwa wanafunzi shuleni ambao hawajapa fursa ya kufika katika hifadhi hiyo.

“Elimu hii tuliyoipata hapa leo tutahakikisha inakua endelevu kwa kuitoa shuleni kwa wanafunzi wetu ili mazingira na misitu yetu iendelee kuleta tija kwa vizazi vya sasa na baadaye,” alisema.

Wanafunzi wa shule hizo walisema taaluma waliyopewa ni muhimu kwao na watakuwa mabalozi wazuri kuhakikisha misitu inalindwa na kujifadhiwa ili kuepukana na athari za mmomonyoko wa ardhi.

Kaulimbiu ya mwaka huu katika maadhimisho ya Siku ya Misitu Duniani ni ‘Misitu ni Ubunifu, ni Suluhisho jipya kwa Dunia Bora’.




Meneja Uchunguzi wa Kampuni ya Vodacom Tanzania Plc, Joseph Mnyune, akizungumza kuhusu mikakati na jitihada zinazochukuliwa na kampuni hiyo ili kudhibiti ulaghai na uhalifu mtandaoni, wakati wa mkutano ulioandaliwa na Taasisi ya Wataalamu wa Udhibiti wa Rushwa na Ufisadi Tanzania (ACFE-T), mjini Zanzibar mwishoni mwa wiki. Kulia ni Rais wa ACFE Tanzania, Ali Mabrook. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mariam Mwinyi akumbusha utoaji sadaka mwezi Mtukufu

**Na Mwandishi Wetu**

MKE wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariam Mwinyi amesema, sadaka sio lazima kutolewa kipindi cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani, bali hata siku za kawaida zinaongeza upendo na kuigusa jamii yenye uhitaji.

Mama Mariam Mwinyi ambaye ni Msarifu na Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora Foundation (ZMBF), aliyasema hayo kwa nyakati tofauti kwenye ziara yake aliyowakilishwa na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Anna Athanas Paul, alipowatembelea wazee wanaolelewa na serikali, Welezo na Sebleni, watoto yatima waliopo Kijiji cha SOS na Mazizini, pamoja na kituo cha kulelea watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu, kilichopo Fuoni Mambosasa (ZASO), Mkoa wa Mjini Magharibi ambako aliwasalimia, kuwafariji na kuwapa zawadi ya futari.

Aliitaka jamii kujitahidi kufanya ibada ndani ya mwezi Mtukufu wa Ramadhan na kutoa sadaka kwa wingi hasa kuwafikia watu wenye mahitaji maalumu wakiwamo wazee, watoto yatima, wenye ulemavu na maskini ili kupata radhi za Mwenyezi Mungu.

“Kama kawaida desturi yetu mwezi wa Ramadhan huwa tunatembeleana, kujuliana hali, sio desturi pekee, lakini ni maagizo kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, anatutaka waja wake kutoa sadaka kwa wingi na kufanya zaidi mambo mazuri ya kumridhisha yeye, kama kuwakumbuka wazee, wajane, watu wasiojiweza na maskini kuwapa sadaka ili nao watekeleza vizuri ibada hii ya mwezi mtukufu wa Ramandani,” alisema.

Alisema, serikali katika kuyaenzi matunda ya Mapinduzi bado inaendelea kuwajali na kuwaenzi wazee kwenye nyumba maalumu pamoja na watoto yatima ambao serikali inawaangalia kwa jicho la karibu.

Mkurugenzi wa Idara ya Ustawi wa Jamii na Wazee, Hassan Ibrahim Suleiman na Mkurugenzi wa kituo cha kulelea watoto yatima SOS, Asha Salum Ali, walisema msaada alioutoa kwa wazee na watoto hao umewafikia wakati sahihi.

Walisema, licha ya serikali kutoa huduma kama hizo kila mwezi katika jitihada zake za kuwaenzi na kuwatunza watu wenye mahitaji maalum, pia msaada huo alioutoa Mariam Mwinyi utaongeza tija na kuwasaidia wakati huu wenye uhitaji.

Miongoni mwa msaada waliopatiwa wazee na watoto hao ni pamoja na tende, vyakula vikiwamo mchele, unga wa ngano, sembe, mafuta ya kupikia, sukari pamoja na nafaka.

Katika hatua nyingine, Makamu wa Pili wa Rais Hemed Suleiman Abdullah, amejumuika pamoja na wananchi wa mikoa miwili ya Pemba kwa ajili ya futari na kuwataka wananchi kudumisha umoja na ushirikiano baina yao na kusaidiana kwa kila hali hasa katika kipindi hiki cha mfungo chenye fadhila nyingi ndani yake.

Aliwataka Wazanzibar kuienzi rasilimali ya amani na utulivu iliyopo nchini na ndio tunu ya Watanzania ambayo baadhi ya nchi wameikosa na kwamba lazima kuitunza na kuienzi ili kuwarahisishia viongozi wakuu kuyatekeleza kwa vitendo yote waliyo yaahidi kwa wananchi wake.

# Sekta ya utalii yaingiza tril. 8/- mwaka mmoja

**Na Halfani Chusi**



SEKTA ya utalii imeingiza zaidi ya Sh. trilioni nane mwaka 2023, Waziri wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki (pichani) amesema.

Amebainisha kuwa kiasi hicho cha fedha ni matokeo ya jumla ya watalii milioni 1.8 walioingia nchini.

Angellah alibainisha hayo juzi mkoani Dar es Salaam alipozungumzia mafanikio ya miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan katika sekta hiyo.

Alisema mapato hayo na idadi hiyo ya watalii ni makubwa zaidi kuwahi kufikiwa kwenye historia ya nchi, Shirika la Umoja wa Mataifa la Utalii (UNWTO) likiitaja Tanzania ni miongoni mwa nchi ya 11 ambazo zimeongeza idadi kubwa ya watalii baada ya janga la UVIKO-19.

"Wote tutakumbuka wakati ambao nchi yetu ilipitia janga la UVIKO-19 na kwenye hili ningependa kutolea mfano Mkoa wa Arusha ambapo watu wengi wamepoteza ajira kutokana na kushuka kwa idadi ya watalii.

"Lakini baada ya Rais kuingia madarakani, alichukua hatua kwa kuweka afua mbalimbali za kupunguza athari za UVIKO-19," alisema.

Waziri huyo alisema mapato yatokanayo na utalii yameongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 2.57 mwaka 2022 hadi kufikia Dola bilioni 3.37 (zaidi ya Sh. trilioni 8.5) mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 33.5.

"Mwaka 2021, wakati Rais Samia alipoingia madarakani, tulikuwa tumepokea watalii kutoka nje ya nchi 922,692, mwaka 2022 waliongezeka kufika 1,454,920 na mwaka 2023, walifika 1,808,205," alifafanua.

Alisema kuwa Rais Samia alipoingia madarakani mwaka 2021/22, bajeti ilikuwa ni Sh. bilioni 572.2. Mwaka 22/2023 bajeti imeongezwa mpaka kufikia Sh. bilion 627.1 na mwaka huu wa fedha (2023/24) wanatekeleza bajeti ya Sh. bilioni 654.6.

Alisema Wizara ya Utalii imeboresha na kujenga viwanja vya ndege vinne katika hifadhi za taifa kama vile Mikumi, Nyerere, Ruaha (viwanja viwili) na ujenzi wake umefikia asilimia 35.8.

Alisema ujenzi huo unatarajiwa kukamilika Agosti mwaka huu na maboresho hayo katika hifadhi yamewezesha ongezeko kubwa la ndege kutua kutoka 4,482 mwaka 2021 hadi 9,172 mwaka 2023 na kuongeza idadi ya watalii kutoka 113,501 kwa mwaka 2021 hadi 218,274 kwa mwezi Januari 2024. Ni ongezeko la asilimia 94.

Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Hassan Abbasi alisema filamu ya Tanzania The Royal Tour imewezesha kuyafikia masoko makubwa kwa njia za kidigitali na imewekwa kwenye Amazon Prime na itakaa huko milele.

"Mimi ninafikiri hayo ni mafanikio makubwa sana, hakuna 'content' kutoka Tanzania tangu uhuru wetu imewekwa kwenye Amazon Prime, mtandao mkubwa zaidi duniani unaotazamwa na zaidi ya yatu milioni 240 kwa mwaka.

"Lazima tupongeze maono makubwa ya Tanzania The Royal Tour kwa sababu Rais Samia aliona mbali sana. Alichokifanya ni kuitangaza Tanzania duniani, ninaamini The Royal Tour imefungua milango mingi sana.

Kamishina wa Uhifadhi wa Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), Prof. Dos Santos Silayo, alisema ubunifu walioweka kwenye misitu umetokana na chachu iliyoletwa na filamu ya Tanzania The Royal Tour.

Mbunge wa Kawe, Askofu Josephat Gwajima, alisema aliposafiri kwenda Japan mwaka jana, Wajapan walitaka kujua nchi anayotoka, akawaonyesha kwenye ramani wakashindwa kuitambua.

"Mwaka huu Wajapan walewale waliponiuliza ninatokea nchi gani, nikawaambia Tanzania, mmoja akafungua 'iPad' yake na kusema 'Royal Tour', na mimi nikasema, ndio 'Royal Tour', yaani nchi ninayotoka inaitwa Royal Tour. Kwa kweli nilishangaa sana kuona namna gani filamu hii imeitangaza nchi yetu kwa kiasi kikubwa hicho," alisema.

## Mwanajeshi adaiwa kutishia wananchi kwa risasi, DC aonya

**Na Beatrice Shayo**

MKUU wa Wilaya ya Kilosa, mkoani Morogoro, Shaka Hamdu Shaka, amemwonya mwanajeshi mstaafu, Khamis Ndemeka, ambaye anadaiwa kusababisha mgogoro wa ardhi na kumtaka aache kutumia cheo chake kutishia maisha wananchi.

Shaka alifikia uamuzi huo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na wananchi wa kijiji cha Mbekesela, Kata ya Kisanga, wilayani humo kuhusiana na mgogoro huo.

Awali, wananchi walilalamikia kutishiwa maisha wakitaka kuendeleza ardhi yao na kushikiwa panga na mwanajeshi huyo huku akiwatambia kuwa hawamwezi kwa chochote kwa kuwa ana fedha na risasi.

Shaka alisema viongozi waliotangulia walishafanya uamuzi sahihi na vyombo vyote vya ulinzi na usalama vinatakiwa kusimamia uamuzi huo hakuna mabadiliko katika mgogoro huo.

"Panapolalamikiwa ni hapo hapo, walalamikaji ni wale wale, kinacholalamikiwa ni hicho hicho. Kilichofanyiwa uhakiki na serikali ndicho hiki hiki hakuna kilichobadilika. Hatuna jipya la kuja kulifanya lazima tuheshimu uamuzi wa viongozi wetu.

"Wananchi na huyo mwanajeshi hakuna mgogoro hapa ninaviagiza vyombo vya ulinzi na usalama yeyote atakayekuwa kiashiria cha uvunjifu wa amani chukueni hatua za kisheria," alisema.

Shaka alisema Ndemeka ndiye anayeonekani mkorofi na yeye anataka kuvunja amani jambo ambalo haliwezi kukubalika.

"Vyombo vya dola mmelalamikiwa hebu sasa simameni kwenye kufuata sheria. Tendeni haki na mkitenda haki hakutakuwa na malalamiko. Vurugu iliyopo hapa ni ya Lembeka huyo Ndemeka gani bwani? Haiwezekani mtu mmoja atishie usalama wa eneo lote hili kwa kuwa yeye ni nani?" alihoji.

Shaka aliwaomba kila mmoja kuhakikisha anaheshimu sheria na kufuata utaratibu uliowekwa kwa maslahi ya nchi na sio uonevu wa raia.

"Usitake kujifanya wewe una makucha na kutaka kumparamia kila mtu. Hii si vizuri, niwaombe wananchi ishini kwa upendo hii ardhi tutakufa na kuiacha," alisema.

Alisema mgogoro huo wa ardhi kila anapokuja kiongozi mpya unaibuka na kutaka uanze upya jambo ambalo haliwezi kukubalika kwa sababu lilishatolewa uamuzi.

Shaka alisema migogoro ya ardhi imeshika kasi kuliko ile ya wakulima na wafugaji.

"Tumefanya jitihada kubwa ya kupambana na migogoro ya wakulima na wafugaji tunamshukuru Mungu haijamalizika lakini imepungua kwa kiasi kikubwa na kupungua kwake imetutoa kwenye mauaji," alisema Shaka.

Shaka alisema takwimu za miaka mitano ya nyuma kuhusiana na migogoro ya wakulima na wafugaji zinaonyesha kuwa kwa mwaka 2023 hakuna kifo kinachosababishwa na wakulima na wafugaji.

Alisema wametoka kwenye zaidi ya vifo 10 mpaka sasa hakuna vifo na hizo ni jitihada za serikali na wananchi kwa kushirikiana kuondoa changamoto hiyo.

"Mkulima amheshimu mfugaji na mfugaji anatakiwa kumheshimu mkulima. Nyie wote mnahitajiana. Wilaya ya Kilosa asilimia 88 kipato chetu kinategemea kilimo, ukienda kwenye ufugaji ni asilimia tisa," alisema Shaka.

Alisema wakulima wanachangia zaidi ya Sh. milioni 280 kwa mwaka makusanyo ya mapato na wafugaji wanachangia Sh. milioni 73, hivyo utegemezi mkubwa uko kwenye kilimo.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya MASWA.

Kituo cha NYALIKUNGU mkoa wa SIMIYU

Usimamizi wa Mirathi Na.12/2024

KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA

MAREHEMU MOHAMED YAHAYA WA MWAMAPALALA.

KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA RICHARD SAMWEL NYOROBI

TANGAZO

(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslah yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikw kuja kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufany hivyo mnamo tarehe 25 Mwezi 3 Mwaka 2024 kabla huy mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia:

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehem anaweza kuleta mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo tarehe 11 Mwezi 03 Mwaka 2024.

MAHAKAMA YA MWANZO NYALIKUNGU MASWA

HAKIMU

HAKIMU MKUU MAHAKAMA YA MWANZO

IN THE DISTRICT COURT OF BAHI
AT BAHI

PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 3991 OF 2024

In the matter of the Estate of the late ADOLF AMOS KAJ of Nhome – Bahi within Dodoma Region

AND

IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY AMOS KAJI BUJIMU

GENERAL CITATION
(Rule 75 of Probate Rules Gn.369 of 1963)

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estat of the above named deceased are hereby cited to com and see the proceedings if they think fit before the grant o letters of Administration is made to the above name Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 1 Day of 04, 2024

Dated at Dodoma this 18 Day of 03, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE BAHI.

KUPOTEA KWA CHETI



**JACKSON VALENTINE MARANDU** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0692 0075**, kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ROSMINI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2018. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/UBU/40143/2024**

IN THE DISTRICT MAGISTRATE COURT OF DODOMA
AT DODOMA

PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE N. 4565 OF 2024

In the matter of the Estate of the late of the late ZABRON SAULI MWAKASEGE

AND

IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY JONATHAN ZABRON MWAKASEGE

GENERAL CITATION
(Rule 75 Of Probate Rules Gn. 369 of 1963)

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estat of the above named deceased are hereby cited to com and see the proceedings if they think fit before the grant o letters of Administration is made to the above name Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the Day of 4, 2024

Date at Dodoma this 18 Day of 3, 2024.

PETITIONER

PRINCIPAL/SENIOR /RESIDENT MAGISTRATE

KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MWAMBA MOHAMEDI MWAMBA** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba **MC 656 AGG.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**PHQ/TAN/TAN/2084/2024**

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO

SHERIA YA UMILIKISHAJI
WA ARDHI YA MWAKA 1999
NIA YA KUTOA HATI MILIKI

MMILIKI ALIOANDIKISHWA: KURWA MAMBALI RUWAICH PAUL S.L.P 289 MOROGORO

ARDHI: KIWANJA NA. 338 KITALU 'D' OPPOSITE INDUSTRIAL COMPLEX MANISPAA YA MOROGORO

ANAYEOMBA UMILIKI: REVOCATUS PAUL KAPOKOLO, S.L.P 928, MOROGORO

Taarifa inatolewa kwamba **HATI MILIKI YA KUMILIKI ARDH** iliyotajwa hapo juu ilikuwa inamilikiwa na **KURWA MAMBAL RUWAICH PAUL** ambapo mteja huyu aliuza ardhi hiyo kwa **REVOCATUS PAUL KAPOKOLO.**
Hati hii imekwisha muda wake hivyo Ofisi haikusudii kuhuish hati kwa **KURWA MAMBALI RUWAICH PAUL** kwani alikuw ameshauza kiwanja hiki kwa **REVOCATUS PAUL KAPOKOLO.**

Kwahiyo iwapo hakuna pingamizi litakalo tolewa kwa muda w mwezi mmoja toka tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katik gazeti. Kiwanja hiki kitamilikishwa kwa **REVOCATUS PAU KAPOKOLO.**

H.P AMBARA
KNY: MKURUGENZI WA MANISPAA MOROGORO

# Miaka mitatu ya Mama Samia, ZRA yajivunia uwepo wa viongozi wa kitaifa

**Na Mwandishi Wetu**

UNAPOZUNGUMZIA mafanikio ya miaka mitatu ya uongozi wa Rais Dk Samia Suluhu Hassan visiwani Zanzibar yanakwenda sambamba na mafanikio ya miaka mitatu ya uongozi wa Rais wa Zanzibar Dk Hussein Ali Mwinyi.

Mamlaka ya mapato Zanzibar (ZRA) inajivunia uwepo wa viongozi hao wa kitaifa ambapo imesaidia mamlaka hiyo kuongeza ukusanyaji wa mapato visiwani Zanzibar.

ZRA kwa kipindi cha miaka mitatu imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 1.244 Trilioni ambapo kwa mwaka wa kwanza wa uongozi wa DK .Hussein Ali Mwinyi kutoka (Julai 2020 hadi Juni 2021) ZRA iliweza kukusanya shilingi bilioni 304.342.

Kwa Mwaka wa pili kutoka Julai 2021 hadi Juni 2022) ilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 374.760, sawa na ukuaji wa asilimia 23.14 kulinganisha na makuisanyo ya mwaka wa kwanza wa 2020/2021.

Aidha kwa mwaka wa tatu kutoka Julai 2022 hadi Juni 2023 pia ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 565.890 kulinganisha na mapato ya mwaka wa pili wa uongozi wake. Ambapo kwa mwaka wa tatu yamekua kwa asilimia 51.19.

**LENGO LA KUANZISHWA KWA MFUMO WA KIELEKTRONIKI**

Lengo kuu la kuanzisha mfumo huu ni kushajihisha utolewaji wa risiti za kielektroniki ili ZRA kupata mauzo yanayofanyika na kodi inayostahiki kulipwa.iwe inalipwa na kila mlipakodi na kuongeza uwajibikaji wa kulipa kodi kwa hiari.

Mfumo huo ulianza kazi kwa majaribio mnamo mwezi wa Aprili mwaka 2021 na kuanza kazi rasmi mwezi Julai 2021, na hadi kufikia mwezi Julai 2023 imepata mafanikio mengi ikiwemo Kuweza kusajili walipakodi 7,808, kusajili vifaa vya kutolea risiti za kielektroniki (POS) 8,524, mapato kukua kwa asilimia 85.94 katika mwaka wa tatu wa Uuongozi wa Awamu ya nane ikilinganishwa na mwaka wa kwanza 2020/2021.

Mafanikio mengine ni kupitia taarifa za Mfumo wa VFMS,ZRA inatumia taarifa za mfumo kuwapandisha walipa kodi kutoka kulipa kodi ya ushuru wa stempu na kusajiliwa kaika wigo wa kodi ya ongezeko la Thamani (VAT) Baada ya mauzo yao kuangaliwa katika mfumo.

Pia Mfumo umewasaidia wafanyabiashara kuweza kujua mwenendo wa mauzo ya biashara yao na kuomba kuhamishwa kutoka ushuru wa stempu (stamp duty) na kusajiliwa katika wigo wa kodi ya ongezeko la Thamani (VAT) na kutekeleza agizo la Rais wa Zanzibar na mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi la kuuza mashine za VVFD kwa mkopo.

Pia Vituo vya mafuta kufugwa mashine maalumu zinazoitwa Electronic physical pump printers (EFPP) ambapo Zanzibar kuna vituo vya mafuta 87 ,kati ya hivyo 54 vimefungwa mashine maalumu ( EFPP) , na 33 vipo kwenye hatua za kumaliziwa ufungwaji wake. Huku vikiwa vinatumia mashine za kawaida za VFD (POS) katika vituo 54 vilivyofungwa EFPP, Kimoja kipo pemba.

**KUANZISHWA MFUMO WA UKUSANYAJI KODI(ZIDRAS).**

SMZ Kupitia ZRA na eGAZ , imetengeneza mfumo mpya wa ukusanyaji wa Mapato ZIDRAS (Zanzibar Intergrated Domestic Revenue Admintration System) ambapo Mfumo huo umetengenezwa na kampuni ya Kitanzania chini ya usimamizi wa Pamoja na wakala wa serikali Mtandao( E-Government )na ZRA.

Aidha Mfumo huo umeanza kutumika kuanzia mwezi Julai, 2023 kwa kuiwasajili walipakodi wakubwa( large taxpays) kabla ya kuenea matumizi yake kwa walipakodi wote wa Zanzibar.

Pia Mfumo huo una huduma za mtandaoni ambapo Mlipakodi atawajibika kwa kujisajili,kuwasilisha ritani na kufanya malipo bila kufika katika ofisi za ZRA. Hii itawapata wafanyabiashara muda mwingi wa kufanya shughuli zao za kibiashara.

**KUIMARISHA UBORA WA HUDUMA NA KUONGEZA UWAJIBIKAJI WA HIARI**

ZRA katika kuwasogezea huduma wananchi na walipakodi na imeanzisha na kuimarisha Ofisi nne za mikoa katika Mkoa wa Kusini Unguja eneo la Paje, Mkoa wa Kaskazini Unguja katika eneo la Kiwengwa na Mkoa wa Mjini Magharibi katika eneo la Michenzani na Mkoa wa Kaskazini Pemba katika eneo la Wete.

Ofisi hizo zinatoa huduma mbalimbali zikiwemo, utoaji wa leseni za udereva na leseni za njia , usajili wa vyombo vya Moto, upokeaji wa Ritani za walipakodi na nyenginezo.

Pia ZRA imefungua ofisi za huduma (service centres) katika maeneo ya Darajani Mjini Unguja na Nungwi katika Mkoa wa Kaskazini Unguja na imeendelea kuimarisha Ofisi za ZRA Mkoani na Wete Pemba ambazo hivi sasa zinatoa huduma mbalimbali za kikodi kulinganisha na hapo awali.

Hata hivyo ZRA iliamua kujenga jengo lake la Ofisi kwa upande wa pemba, jengo hilo limejengwa katika eneo la GOMBANI limezinduliwa na Dkt Hussein Ali Mwinyi na kuanza kazi rasmi mnamo mwezi wa September 2021 na kuwepo kwa jengo hilo , imekuwa ni Faraja kwa walipakodi wa Pemba ambao wanapata huduma katika mazingira bora zaidi.

Aidha ZRA imeimarisha utoaji wa elimu kwa walipakodi kwa njia mbalimbali zikiwemo Mikutano na Walipakodi,Semina ,Makongamano, Machapisho mbalimbali katika vyombo vya Habari na inatumia mitandao ya kijamii katika kufikisha elimu na jumbe mbalimbali kwa walipakodi ili kuhamasisha ulipaji kodi wa Hiari Zanzibar.

ZRA imeanzisha na kusajili ZRA ONLINE TV Kwa lengo la kuhabarisha na kuhamasisha ulipaji kodi wa Hiari Zanzibar.

ZRA
ZANZIBAR REVENUE AUTHORITY

MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR

SALAMU ZA PONGEZI

UONGOZI PAMOJA NA WAFANYAKAZI WOTE WA MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR (ZRA).WANAUNGANA NA WATANZANIA WOTE KUMPONGEZA RAIS WA JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA **MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN** KWA KUTIMIZA MIAKA 3 YA UONGOZI WAKE .

KIPEKEE KABISA ZRA INAMSHUKURU KWA DHATI RAIS WETU MPENDWA KWA KUWA MUHAMASISHAJI NAMBARI MOJA WA UTALII NCHINI NA KUTUONGEZEA MAPATO KUPITIA SEKTA YA UTALII.

***"TULIPE KODI KWA MAENDELEO YA ZANZIBAR"***



**Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**Zanzibar Revenue Authority (ZRA),**
**P. O, BOX 2072, Mazizini- Zanzibar,**
**Tel: 255-24-2230639/2233041,**
**Fax: 255-24-2233904, Email: zrb@zanrevenue.org**

**ZRA Pemba Office**
**S.L.P 163, Pemba, Zanzibar.**
**Tel: +255 24 2452553, Fax: +255 24 2452945**

HABARI MICHEZO

# MABONDIA WA TANZANIA WAENDELEA KUFAVYA VIZURI ALL-AFRICAN GAMES

**Na Saad Akida**

BENDERA ya Tanzania imeendelea kupeperushwa vema nchini Ghana kwenye michezo ya Afrika (All-African Games), upande wa masumbwi baada ya Bondia, Ezra Paulo, kufanikiwa kutinga nusu fainali.

Paulo juzi alikuwa na kibarua kigumu na kumshinda mpinzani wake Mujinga Frazier, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) kwa pointi 5-0 katika uzito wa Light kwenye Ukumbi wa Bukom Arena jijini Accra.

Lilikuwa pambano namba 74 uzani wa Light Weight Kg 60, ambalo Ezra alicheza kwa ustadi wa hali ya juu na kuwashawishi majaji wote watano kumpa ushindi na kutinga hatua ya nusu fainali.

Ezra anakuwa bondia wa pili kuhakikishia Tanzania inapeperusha vema bendera yake kwenye michezo All-African Games, Accra 2023 inayoendelea katika jiji hilo nchini Ghana.

Hiyo ni baada ya Jumapili iliyopita bondia wa Timu ya Taifa ya Tanzania wa Ngumi za Ridhaa, Yusuf Changalawe, kutinga robo fainali ya baada ya kumshinda Abdelgawwad Orabi Salah wa Misri kwa pointi katika uzito wa Light Heavy.

Ezra sasa atacheza hatua ya nusu fainali dhidi ya Andrew Chilata kutoka Zambia na hata kama atapoteza tayari ana uhakika wa kupata medali ya Shaba, ambayo hutolewa kwa wote waliotinga hatua ya nusu fainali.

Hiyo ikiwa ni medali ya pili kwani bondia wa kwanza kuihakikishia Tanzania ni Mussa Maregesi wa uzani wa Cruiser Weight Kg 86 ambaye tayari yupo hatua ya nusu fainali.

SOKA...




Vijana wakicheza mpira katika Uwanja wa Shule ya Msingi Kivule, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kipre kinara ‘asisti’, Matampi ‘clean sheets’

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI viungo washambuliaji wawili, Stephane Aziz Ki wa Yanga na Feisal Salum ‚Fei Toto‘ wa Azam FC wakiongoza kwenye orodha ya wafungaji wa Ligi Kuu, kila mmoja akiwa na mabao 13, winga wa Azam FC, Kipre Junior, anaongoza kwa kutoa pasi nyingi zilizozaa mabao (‚asisti‘), huku kipa wa Coastal Union, Ley Matampi, akiwa kinara wa kukaa langoni mechi nyingi bila kuruhusu bao.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa jana na Bodi ya Ligi, Kipre anaongoza mpaka sasa akiwa ameshafikisha ‚asisti‘ nane.

Jumapili iliyopita, mchezaji huyo raia wa Ivory Coast, alitoa ‚asisti‘ kwa mfungaji wa bao la kwanza dhidi ya Yanga, Gibril Sillah na kutimiza idadi hiyo katika mechi ambayo Azam ilishinda mabao 2-1, ikichezwa Uwanja wa Banjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Mchezaji huyo anafuatiwa na Muivory Coast mwenzake, Yao Kuoassi na Mburkina Faso Aziz Ki, wote wa Yanga ambao wana ‚asisti‘ saba kila mmoja.

Jumla ya wachezaji watano wanashika nafasi ya tatu kwa kuwa na ‚asisti‘ nyingi kwenye Ligi Kuu, wakifanya hivyo mara tano, nao ni Clatous Chama wa Simba, Impiri Mbombo wa Tabora United, Awesu Awesu na Rahim Shomari, wote wa KMC.

Naye kipa wa Coastal Union, Mkongomani, Matampi, anaongoza akifikisha ‚clean sheets‘ 10 mpaka sasa.

Anafuatiwa wa Djigui Diarra wa Yanga mwenye ‚clean sheets‘ nane, John Noble wa Tabora United na Costantine Malimi wa Geita Gold ambao wanazo saba kila mmoja, Jonathan Nahimana wa Namungo na Yona Amosi wa Prisons wakiwa na sita, Ayoub Lakred wa Simba na Ramadhani Chalamanda wa Kagera Sugar wakikaa mara tano langoni bila wavu kugushwa na Wilbol Maseke wa KMC, akiwa na nne.

# Ihefu yakimbilia tena jijini Arusha

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Ihefu FC, kilitarajiwa kuondoka jana mkoani Singida kwenda jijini Arusha kwa ajili ya kuweka kambi kujiandaa na michezo inayokuja ya Ligi Kuu na Kombe la FA.

Timu hiyo imeamua kwenda Arusha baada ya kupoteza mechi zake mbili za Ligi Kuu, ikifungwa mabao 5-0 dhidi ya Yanga, Machi 11, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam na bao 1-0 dhidi ya Coastal Union, Machi 14, Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Peter Andrew, amesema wanaelekea Arusha si kwa sababu zingine zozote bali ni kwa ajili ya urahisi wa kupata mechi za kirafiki tofauti na kama wangepiga kambi Singida.

“Singida ni nyumbani, lakini kama unakumbuka tuliweka kambi Arusha kwa muda kipindi tunajiandaa na mechi za mzunguko wa pili wa Ligi Kuu, Singida si kama ni sehemu mbaya ya kufanya maandalizi, ila kule Arusha tuna nafasi pana ya kupata michezo ya kirafiki, kuna timu nyingi za daraja la kwanza, Mbuni FC, TMA, kwa hiyo tunaweza kupata mechi mbili tatu, kitu ambacho kinatupa ugumu sana tukiwa hapa, hakuna timu za madaraja ambayo yanaweza kutupa changamoto,“ alisema ofisa habari huyo.

Aliitaja sababu nyingine ni kwamba wana mechi nyingi watazocheza nje ya uwanja wao wa nyumbani, hivyo wanakwenda ugenini ili kuzoea mazingira pia.

“Kitu kilichopo ni kwamba tuna michezo mingi ya ugenini, kwa hiyo tunakwenda Arusha ili kupata uzoefu zaidi ya kucheza ugenini, baada ya hapo tutaanza kuzunguka kuanzia Dar es Salaam na sehemu zingine, tukimaliza mechi hizo ndiyo tunarudi kujikita nyumbani Singida,“ alisema Peter.

Ihefu hivi sasa imehamia mkoani Singida na inacheza mechi zake kwenye Uwanja wa Liti, Singida, huku ikipishana na Singida Fountain Gate ambayo imehama mkoani humo ikielekea Mwanza, na kupiga mechi zake za Ligi Kuu, Uwanja wa CCM Kirumba jijini humo.

Timu hiyo ipo nafasi ya 11 ya msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa na pointi 23 mpaka sasa.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**NEWCASTLE KUMUUZA BRUNO**

KLABU ya Newcastle United inafikiria kumuuza kiungo wa kati wa Brazil, Bruno Guimaraes mwenye umri wa miaka 26, ili kufadhili matumizi yao ya msimu wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

**MADRID, PSG WAMFUATILIA**

REAL Madrid na Paris St-Germain walikuwa wakimtazama Bruno Guimaraes, katika kichapo cha Jumamosi cha Kombe la FA kutoka kwa Manchester City, huku PSG pia wakifuatilia kwa karibu mmoja wa wachezaji wenzake wa Newcastle - mshambuliaji wa Sweden, Alexander Isak, 24. ***(HITC)***

**KIMMICH KUPELEKWA SOKONI**

BAYERN Munich ipo tayari kumuuza kiungo wa kati wa Ujerumani, Joshua Kimmich, msimu huu wa majira ya joto, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, anataka tu kujiunga na Manchester City, Arsenal, Liverpool, Real Madrid au Barcelona. ***(Florian Plettenberg)***

**DIAZ AWANIWA LIVERPOOL**

MANCHESTER United na Liverpool ni miongoni mwa klabu zinazotaka kumsajili mshambuliaji wa Real Madrid na Morocco, Brahim Diaz mwenye umri wa miaka 24. ***(HITC)***

**SILVA KUREJEA BENFICA**

KIUNGO wa kati wa Manchester City na Ureno, Bernardo Silva, amesema ana uhakika atarejea katika klabu yake ya kwanza ya Benfica, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 alikataa kusema lini. ***(SIC)***

**BRANTHWAITE BEI JUU**

EVERTON itahitaji kima cha chini cha pauni milioni 80 kumnunua mlinzi wa England, Jarrad Branthwaite mwenye umri wa miaka 21, ambaye anasakwa na Manchester United na Chelsea. ***(Team Talks)***

**STERLING HAITAKI SAUDIA**

MSHAMBULIAJI wa England, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 29, atakataa nia kutoka Klabu za Saudi Arabia msimu huu wa majira ya joto. ***(Standard)***

**PALMER KUZAWADIWA**

CHELSEA inatazamia italazimika kumzawadia fowadi wa England, Cole Palmer mwenye umri wa miaka 21, mkataba mpya na masharti yaliyoboreshwa baada ya kuanza maisha vizuri Stamford Bridge. ***(Football Insider)***

**NKETIAH KUONDOKA ARSENAL**

MCHEZAJI Eddie Nketiah huenda akaondoka Arsenal msimu huu wa majira ya joto na Wolves wamejiunga na Klabu za Ligi Kuu England wakiwinda uwezekano wa kumnunua mshambuliaji huyo wa England mwenye umri wa miaka 24. ***(Teamtalk)***

**JOHNSON AWANIWA SPURS**

KLABU ya Tottenham Hotspur imeelekeza macho yake kwa beki wa pembeni wa West Ham, Ben Johnson mwenye umri wa miaka 24. ***(Football)***

**HINCAPIE ATAKIWA LIVER**

LIVERPOOL imeongeza nia ya kumnunua beki wa upande wa kushoto wa Bayer Leverkusen, Piero Hincapie, ambaye ni mchezaji wa Kimataifa wa Ecuador mwenye umri wa miaka 22. ***(HITC)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# SABABU ARGENTINA KUMWACHA MESSI

Aungana na Dybala, sasa wataikosa Costa Rica na Salvador hii ni baada ya...

**BUENOS AIRES, Argentina**

LIONEL Messi atakosa mechi zijazo za kirafiki za Argentina dhidi ya El Salvador na Costa Rica kwa sababu ya jeraha la msuli wa paja la kulia, shirikisho la soka la nchi hiyo limesema.

Nahodha huyo wa Argentina alibadilishwa mapema katika kipindi cha pili cha ushindi wa mabao 3-1 wa wiki iliyopita dhidi ya Nashville kwenye Kombe la Mabingwa wa Concacaf kwa sababu ya jeraha hilo na alikaa nje ya ushindi wa ligi Jumamosi dhidi ya D.C. United.

Kocha wa Inter Miami CF, Gerardo „Tata" Martino, alisema baada ya mchezo huo kuwa hali ya Messi itatathminiwa „wiki baada ya wiki."

Messi mwenye umri wa miaka 36, awali alikuwa amejumuishwa kwenye kikosi cha Argentina kwa mechi za kirafiki za kimataifa dhidi ya El Salvador mjini Philadelphia Ijumaa hii, na dhidi ya Costa Rica mjini Los Angeles siku nne baadaye, lakini hilo limebadilika.

ESPN Argentina iliripoti kwamba Messi bado anaweza kuungana na timu ya taifa baadaye wiki hii ili kufanyiwa sehemu ya mchakato wake wa kupona kabla ya kurejea Florida.

Wachezaji kadhaa wa Argentina, akiwamo mshambuliaji wa Manchester City, Julian Alvarez, waliwasili Philadelphia Jumapili, huku wachezaji wengine wa kikosi wakitarajiwa kuungana nao jana.

Michezo yote miwili ni ya maandalizi kwa Mabingwa Watetezi, Argentina kwa Copa America Juni na Julai, ambayo pia itakuwa nchini Marekani.

Argentina tayari ilikuwa imewapoteza mshambuliaji Paulo Dybala na kiungo wa kati Exequiel Palacios kutokana na majeraha.

# MADRID YALALAMIKIA UBAGUZI KWA VINICIUS

**MADRID, Hispania**

REAL Madrid imetangaza kuwasilisha malalamiko yao dhidi ya mwamuzi Juan Martinez Munuera "kwa hiari na kwa makusudi" kupuuza unyanyasaji wa kibaguzi wa winga Vinicius Junior.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Brazil ni mmoja wa wachezaji nyota wa Madrid, lakini amekuwa mwathirika wa matukio kadhaa ya ubaguzi wa rangi tangu alipohamia Hispania.

'Los Blancos' hao sasa wamemshutumu Munuera kwa kukataa kwa makusudi unyanyasaji wa kibaguzi wa Vinicius wakati wa ushindi wa mabao 4-2 Jumamosi dhidi ya Osasuna, ambapo mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, alifunga mara mbili.

Taarifa kutoka Madrid ilisema: "Baada ya matusi mazito yaliyotolewa, kwa mara nyingine tena, dhidi ya mchezaji wetu Vinicius Junior, katika kesi hii wakati wa mechi ya mwisho ya ligi iliyochezwa na timu yetu huko El Sadar, Real Madrid CF inawasilisha yafuatayo.

"Klabu yetu imewasilisha malalamiko kwenye kamati ya nidhamu ya Shirikisho la Soka la Hispania dhidi ya mwamuzi wa mchezo Juan Martinez Munuera, kutokana na uzembe wa kuandaa ripoti. Mwamuzi huyu kwa hiari yake na kwa makusudi aliacha matusi na kelele za fedheha zilizoelekezwa mara kwa mara kuelekea kwa mchezaji wetu Vinicius Junior, licha ya kuonywa kwa msisitizo na wachezaji wetu.

"Pamoja na hayo, Real Madrid pia imewasilisha malalamiko kwenye chombo hiki cha shirikisho kuhusiana na matusi na kelele za udhalilishaji zilizotajwa hapo juu, na imeyapeleka kwenye Tume ya Taifa ya Kupambana na Ukatili, Ubaguzi na Kutovumiliana Michezoni, ili waliotamka watambuliwe na kuadhibiwa."

Vinicius kwa muda mrefu amekuwa mwathirika wa unyanyasaji wa ubaguzi wa rangi nchini Hispania.

Wanaume wanne walikamatwa Mei 2023 kwa kutundika sanamu ya winga huyo kwenye daraja la Madrid.

Mwezi huo wakati wa mchezo wa LaLiga dhidi ya Valencia kwenye Uwanja wa Mestalla, Mbrazil huyo alikashifiwa zaidi na kulaani tukio hilo hadharani, na kusababisha mjadala mpana juu ya ubaguzi wa rangi nchini Hispania.

Taarifa ya Madrid imeongeza: "Kwa kuzingatia matukio haya ya kusikitisha yaliyotokea El Sadar, Real Madrid imepanua malalamiko ambayo iliwasilisha Ijumaa iliyopita, Machi 15, kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali dhidi ya uhalifu wa chuki na ubaguzi."




## Felix: Mimi si mbaya kwa Atletico Madrid

**MADRID, Hispania**

JOAO Felix amesisitiza kuwa yeye si "mtu mbaya" katika mzozo wake unaoendelea na klabu yake mama ya Atletico Madrid baada ya kufunga bao dhidi yao akiwa na Barcelona.

Mshambuliaji huyo wa Ureno alijiunga na Barca kwa mkopo katika siku ya mwisho ya dirisha la usajili la majira ya joto 2023.

Alitumia muda mwingi wa dirisha kujaribu kulazimisha kuhamia kwa mabingwa wa Hispania akitaja kama klabu yake ya ndoto ya utotoni.

Sheria ya LaLiga inasema wachezaji wa mkopo wanaruhusiwa kucheza dhidi ya timu yao mama.

Felix alifunga bao pekee katika ushindi wa 1-0 dhidi ya Atletico Desemba mwaka jana kutokana na bao la kwanza katika ushindi wa mabao 3-0 kwa Barcelona Jumapili.

Mashabiki wa Atletico walichafua picha ya Felix nje ya uwanja kabla ya mchezo kabla ya kumzomea na kumpigia miluzi katika muda wote wa dakika 77 alizokuwa uwanjani.

Akizungumza na ESPN baada ya mechi, Felix alidai mashabiki hawajui hadithi kamili kuhusu uhusiano wake na Atletico.

"Mashabiki hapa wanaotazama mchezo hawajui kinachotokea ndani," alisema Felix.

"Wachezaji wenzangu wa Atletico wanajua na, kama unavyoona, ninashirikiana nao wote vizuri.

"Nilisimama kuzungumza na Samuel Lino na Thomas Lemar, huku kila mtu akija kunikumbatia, kuzungumza nami na kuniuliza jinsi familia yangu ilivyo. Sina chochote dhidi yao na hawana chochote dhidi yangu.

"Mwisho wa siku, mimi si mtu mbaya hapa, lakini ninaelewa mashabiki kwa sababu hawajui kila kitu."

Mkataba wa mkopo wa Felix haujumuishi chaguo la kumnunua na isipokuwa makubaliano yatafikiwa kabla ya msimu wa majira ya joto, atalazimika kurejea Atletico kwa ajili ya maandalizi ya msimu kabla ya kampeni ya 2024/25.

Ripoti kutoka Hispania zinaeleza kuwa Barcelona watajaribu kumsajili kwa mkopo mwingine kabla ya kumnunua kwa bei iliyopunguzwa.



## Nunez ajiondoa Uruguay

**LIVERPOOL, England**

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Darwin Nunez, amejiondoa kwenye kikosi cha Uruguay kwa ajili ya mechi zao za kimataifa za Machi kutokana na jeraha.

Nunez alipata jeraha la msuli wa paja wakati 'Wekundu' hao wakichapwa mabao 4-3 na Manchester United kwenye robo fainali ya Kombe la FA Jumapili.

Alikamilisha dakika 120 kamili baada ya muda wa nyongeza na kunyakua pasi ya Alexis Mac Allister, lakini akatoa mpira na kusababisha bao la kusawazisha la Marcus Rashford na kufanya kuwa 3-3.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya mechi, Klopp alithibitisha kuwa Nunez - pamoja na Luis Diaz na Cody Gakpo - walijeruhiwa wakati wa mchezo huo.

"Sasa, wanaendelea na majukumu ya kimataifa. Tunatumai watarejea wakiwa na afya njema. Lucho (Diaz) aliumia paja, Darwin (Nunez) aliumia misuli ya paja. Cody aliumia kifundo cha mguu," alisema Klopp.

Liverpool angalau wametiwa nguvu na habari kwamba Nunez amejiondoa kwenye kikosi cha Uruguay kwa ajili ya mechi za kirafiki mwezi huu kutokana na mazungumzo na Kocha Mkuu, Marcelo Bielsa.

Uruguay wanatarajiwa kucheza na Basque Country XI huko Bilbao na kisha Ivory Coast huko Lens kama sehemu ya ziara ya Ulaya.

Wamepanga mechi moja tu ya kirafiki kabla ya kuanza kwa michuano ya Copa America huko Marekani.



# MADRID YALALAMIKIA UBAGUZI KWA VINICIUS

**MADRID, Hispania**

REAL Madrid imetangaza kuwasilisha malalamiko yao dhidi ya mwamuzi Juan Martinez Munuera "kwa hiari na kwa makusudi" kupuuza unyanyasaji wa kibaguzi wa winga Vinicius Junior.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Brazil ni mmoja wa wachezaji nyota wa Madrid, lakini amekuwa mwathirika wa matukio kadhaa ya ubaguzi wa rangi tangu alipohamia Hispania.

'Los Blancos' hao sasa wamemshutumu Munuera kwa kukataa kwa makusudi unyanyasaji wa kibaguzi wa Vinicius wakati wa ushindi wa mabao 4-2 Jumamosi dhidi ya Osasuna, ambapo mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, alifunga mara mbili.

Taarifa kutoka Madrid ilisema: "Baada ya matusi mazito yaliyotolewa, kwa mara nyingine tena, dhidi ya mchezaji wetu Vinicius Junior, katika kesi hii wakati wa mechi ya mwisho ya ligi iliyochezwa na timu yetu huko El Sadar, Real Madrid CF inawasilisha yafuatayo.

"Klabu yetu imewasilisha malalamiko kwenye kamati ya nidhamu ya Shirikisho la Soka la




Hispania dhidi ya mwamuzi wa mchezo Juan Martinez Munuera, kutokana na uzembe wa kuandaa ripoti. Mwamuzi huyu kwa hiari yake na kwa makusudi aliacha matusi na kelele za fedheha zilizoelekezwa mara kwa mara kuelekea kwa mchezaji wetu Vinicius Junior, licha ya kuonywa kwa msisitizo na wachezaji wetu.

"Pamoja na hayo, Real Madrid pia imewasilisha malalamiko kwenye chombo hiki cha shirikisho kuhusiana na matusi na kelele za udhalilishaji zilizotajwa hapo juu, na imeyapeleka kwenye Tume ya Taifa ya Kupambana na Ukatili, Ubaguzi na Kutovumiliana Michezoni, ili waliotamka watambuliwe na kuadhibiwa."

Vinicius kwa muda mrefu amekuwa mwathirika wa unyanyasaji wa ubaguzi wa rangi nchini Hispania.

Wanaume wanne walikamatwa Mei 2023 kwa kutundika sanamu ya winga huyo kwenye daraja la Madrid.

Mwezi huo wakati wa mchezo wa LaLiga dhidi ya Valencia kwenye Uwanja wa Mestalla, Mbrazil huyo alikashifiwa zaidi na kulaani tukio hilo hadharani, na kusababisha mjadala mpana juu ya ubaguzi wa rangi nchini Hispania.

Taarifa ya Madrid imeongeza: "Kwa kuzingatia matukio haya ya kusikitisha yaliyotokea El Sadar, Real Madrid imepanua malalamiko ambayo iliwasilisha Ijumaa iliyopita, Machi 15, kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali dhidi ya uhalifu wa chuki na ubaguzi."

## Felix: Mimi si mbaya kwa Atletico Madrid

**MADRID, Hispania**

JOAO Felix amesisitiza kuwa yeye si "mtu mbaya" katika mzozo wake unaoendelea na klabu yake mama ya Atletico Madrid baada ya kufunga bao dhidi yao akiwa na Barcelona.

Mshambuliaji huyo wa Ureno alijiunga na Barca kwa mkopo katika siku ya mwisho ya dirisha la usajili la majira ya joto 2023.

Alitumia muda mwingi wa dirisha kujaribu kulazimisha kuhamia kwa mabingwa wa Hispania akitaja kama klabu yake ya ndoto ya utotoni.

Sheria ya LaLiga inasema wachezaji wa mkopo wanaruhusiwa kucheza dhidi ya timu yao mama.

Felix alifunga bao pekee katika ushindi wa 1-0 dhidi ya Atletico Desemba mwaka jana kutokana na bao la kwanza katika ushindi wa mabao 3-0 kwa Barcelona Jumapili.

Mashabiki wa Atletico walichafua picha ya Felix nje ya uwanja kabla ya mchezo kabla ya kumzomea na kumpigia miluzi katika muda wote wa dakika 77 alizokuwa uwanjani.

Akizungumza na ESPN baada ya mechi, Felix alidai mashabiki hawajui hadithi kamili kuhusu uhusiano wake na Atletico.

"Mashabiki hapa wanaotazama mchezo hawajui kinachotokea ndani," alisema Felix.

"Wachezaji wenzangu wa Atletico wanajua na, kama unavyoona, ninashirikiana nao wote vizuri.

"Nilisimama kuzungumza na Samuel Lino na Thomas Lemar, huku kila mtu akija kunikumbatia, kuzungumza nami na kuniuliza jinsi familia yangu ilivyo. Sina chochote dhidi yao na hawana chochote dhidi yangu.

"Mwisho wa siku, mimi si mtu mbaya hapa, lakini ninaelewa mashabiki kwa sababu hawajui kila kitu."

Mkataba wa mkopo wa Felix haujumuishi chaguo la kumnunua na isipokuwa makubaliano yatafikiwa kabla ya msimu wa majira ya joto, atalazimika kurejea Atletico kwa ajili ya maandalizi ya msimu kabla ya kampeni ya 2024/25.

Ripoti kutoka Hispania zinaeleza kuwa Barcelona watajaribu kumsajili kwa mkopo mwingine kabla ya kumnunua kwa bei iliyopunguzwa.



## Nunez ajiondoa Uruguay

**LIVERPOOL, England**

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Darwin Nunez, amejiondoa kwenye kikosi cha Uruguay kwa ajili ya mechi zao za kimataifa za Machi kutokana na jeraha.

Nunez alipata jeraha la msuli wa paja wakati 'Wekundu' hao wakichapwa mabao 4-3 na Manchester United kwenye robo fainali ya Kombe la FA Jumapili.

Alikamilisha dakika 120 kamili baada ya muda wa nyongeza na kunyakua pasi ya Alexis Mac Allister, lakini akatoa mpira na kusababisha bao la kusawazisha la Marcus Rashford na kufanya kuwa 3-3.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya mechi, Klopp alithibitisha kuwa Nunez - pamoja na Luis Diaz na Cody Gakpo - walijeruhiwa wakati wa mchezo huo.

"Sasa, wanaendelea na majukumu ya kimataifa. Tunatumai watarejea wakiwa na afya njema. Lucho (Diaz) aliumia paja, Darwin (Nunez) aliumia misuli ya paja. Cody aliumia kifundo cha mguu," alisema Klopp.

Liverpool angalau wametiwa nguvu na habari kwamba Nunez amejiondoa kwenye kikosi cha Uruguay kwa ajili ya mechi za kirafiki mwezi huu kutokana na mazungumzo na Kocha Mkuu, Marcelo Bielsa.

Uruguay wanatarajiwa kucheza na Basque Country XI huko Bilbao na kisha Ivory Coast huko Lens kama sehemu ya ziara ya Ulaya.

Wamepanga mechi moja tu ya kirafiki kabla ya kuanza kwa michuano ya Copa America huko Marekani.



Michezo
Jumatano Machi 20, 2024
Nipashe

Sababu Argentina kumwacha Messi UKURASA 21



KAMBINI...



Wachezaji wa Simba wakielekea kambini Zanzibar jana kwa kambi ya wiki moja kujiandaa na robo fainali Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly ya Misri. **MPIGAPICHA WETU**


# GAMONDI AICHAMBUA MAMELODI KWA YANGA

●●●Asema ni wakubwa sana kwao, ahoji siwatacheza 11 kwa 11 au? TFF yazibeba...

**Na Saada Akida**

HUKU wengi wakiipa nafasi zaidi Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini kwenye mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Yanga Machi 30, mwaka huu, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, ameichambua timu hiyo na kusema hakuna lisilowezekana kwa kuwa watakuwa 11 kwa 11 uwanjani na si vinginevyo.

Yanga itaikaribisha Mamelodi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa na baada ya hapo timu hizo zitarudiana Aprili 5, mwaka huu, nchini Afrika Kusini na mshindi wa jumla atatinga nusu fainali ya michuano hiyo mikubwa zaidi kwa ngazi ya klabu barani Afrika.



Akiwachambua wapinzani wao hao jana, Gamondi alisema ubora wa kikosi na bajeti ya usajili wa Mamelodi Sundowns tofauti na Yang, lakini hilo haliwapi woga, badala yake wanahitaji kupambana na kuweka juhudi zaidi katika mchezo huo wa nyumbani.

Gamondi alisema anafahamu misingi ya Mamelodi kwa sababu timu yake ya zamani na wamekuwa bora sana kwa msimu huu, na kwamba waliongeza mchezaji kutoka Argentina kwa usajili ghali tofauti na wao ambao dirisha dogo waliwaleta Joseph Guede na Augustine Okrah wakiwa wachezaji huru.

Alisema kuna tofauti kubwa ya Mamelodi Sundowns na timu kubwa kwa Yanga, ila ni wakati maalum kwao kuonyesha ubora na ili kufikia ukubwa huo wa kuwa miongoni mwa timu tano bora Afrika, lazima wapambane kushinda mechi hiyo.

"Tunahitaji kupigana, kuweka juhudi zaidi kuliko Sundowns, kama nilivyosema awali tulipocheza na Al Ahly, suala la uzoefu lilituathiri kidogo, pia bajeti ukilinganisha na yetu ni tofauti, lazima watu waelewe, lakini haijalishi kwani mpira ni dakika 90 na wote tunacheza 11 dhidi ya 11," alisema kocha huyo.

Alisema wanatakiwa kuweka juhudi kubwa kuhakikisha wanapambana na timu bora yenye wachezaji wenye uzoefu mkubwa.

Aliongeza kuwa miaka ya hivi majuzi, Mamelodi Sundowns imekuwa ikipata wapinzani wengi kutoka Afrika Kaskazini katika michuano ya Ligi ya Mabingwa, mara ya mwisho kuwa na upinzani Kusini mwa Jangwa la Sahara ilikuwa msimu wa 2021/22 walipotupwa nje na wababe wa Angola, Petro Atletico, hivyo ni zamu ya Yanga kwa kuhakikisha wanashinda mechi ya kwanza ya nyumbani. Wakati huo huo, Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), limezikubalia klabu za Simba na Yanga kuwaruhusu nyota wa

INAENDELEA UK. 23

## Benchikha na siri Simba kambi Zenji

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Simba kimetua mjini Zanzibar jana kikitokea jijini Dar es Salaam, tayari kwa kambi ya wiki moja kabla ya kuivaa Al Ahly ya Misri kwenye mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, huku klabu hiyo ikieleza sababu ya kukimbilia visiwa hivyo vya karafuu.

Akizungumza jana, Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema wameamua kuelekea kambi Zanzibar kwa ajili ya kupata utulivu ili kumpa muda Kocha Mkuu, Abdelhak Benchikha, kuandaa vizuri programu yake kwani alihitaji mazoezi yawe yanafanyika usiku kwani mechi zote mbili zitachezwa nyakati hizo.

"Watu wanajiuliza kwa nini Zanzibar? Tumeamua kwenda huko mahsusi ili kupata utulivu, kumpa muda mwalimu Banchikha kwa ajili ya kuandaa timu ya kwenda kumtoa Al Ahly na kwanza tumezingatia suala zima la utulivu, mwalimu anasema anahitaji programu ya mazoezi hasa nyakati za usiku kwa sababu mechi zote mbili ya Dar es Salaam na Cairo zitachezwa usiku, tukakaa na kuona Zenji ndiko kuna miundombinu mizuri zaidi," alisema Ahmed.

Alisema wakiwa huko wanataraji kucheza mchezo mmoja wa kirafiki ili mwalimu aangalie kile ambacho amekitengeneza kama kimekuwa tayari, na baada ya hapo kikosi kitakuwa kimekamilika kuwavaa Al Ahly.

"Dhamira yetu safari hii ni kuitoa Al Ahly na kufuzu kwenda hatua ya nusu fainali, tuna vitu viwili, tuna vitu viwili, kumfunga na kumtoa, tushamfunga sana, kipindi cha miaka mitano tumekutana naye mara tatu, na imehusisha mechi sita, katika hizo tumeshinda mbili, ametufunga mbili na tumetoa sare mara mbili pia, kwa hiyo ukiangalia kitakwimu tunalingana, safari hii tunataka kutengeneza utofauti wa kumtoa na inawezekana, ndiyo maana tunataka kufanya maandalizi makubwa," alisema Meneja huyo.

Hata hivyo, zipo taarifa kuwa kikosi kimepelekwa Zanzibar kufuatia ushauri wa wajumbe wa Baraza la Ushauri la Klabu, ambapo mmoja wa

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >